# Nipashe

Alhamisi Machi 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580516

www.ippmedia.com

MWANGA

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US





**Mgomo** wa mabasi warindima, LATRA yawaonya wamiliki

UKURASA 2



**Waziri** Mhagama awashukia waajiri mikataba madereva

UKURASA 3

**Rivaldo aitaka Barcelona sasa kumsajili Ramos**

UKURASA 22

# MAUAJI YA KUTISHA

• **Mali** za jaji zadaiwa kusababisha vifo vya mume, mke... *Endelea Ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**ZANZIBAR YATOA MSIMAMO CHANJO YA CORONA**

WAZIRI wa Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui...

UKURASA WA 7

**MKURUGENZI SHULE MAARUFU AHOJIWA NA TAKUKURU**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imemhoji Mkurugenzi wa...

UKURASA WA 7

**WALIMU WAONYWA KUWEKA ATM REHANI**

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewataka...





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimjulia hali mpigapicha wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hassan Issa, aliyelazwa katika Hospitali ya Mnazimmoja jana, wakati akiwajulia hali majeruhi wa ajali iliyotokea eneo la Kitogani, Mkoa wa Kusini Unguja, wakiwa katika msafara wa Makamu wa Pili wa Rais. Kulia kwake ni Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla. **PICHA: IKULU**

## Serikali yaingilia ubomoaji nyumba

UKURASA 3



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



## Nuru yaonekana kero ulipaji mikopo HESLB

UKURASA 2


**MICHEZO** TWANGA YATANGAZA UZINDUZI ALBAM MPYA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavie (wa pili kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Nchi Wanachama wanaozungumza lugha ya Kifaransa Francophonie. Kushoto ni Balozi wa Switzerland nchini, Didier Chassot, Balozi wa Morocco nchini, Abdelilah Benryane (wa pili kulia) na Balozi wa Canada, Pamela O'donnel. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mauaji ya kutisha ya mume na mke

**Na Waandishi Wetu,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia mtu mmoja huku likiwasaka wengine wawili kwa tuhuma za kuwaua kikatili watu wawili ambao ni mume na mke kisha kutelekeza miili yao katika maeneo tofauti.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliwataja waliouawa kuwa ni Samson Ndavi ambaye alikuwa mlinzi kwenye nyumba ya aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Bethuel Mila, pamoja na mke wa mlinzi huyo, Christina Mwakilembe.

Alisema watu hao waliuawa kwa kupigwa na nondo kichwani kwa siku mbili tofauti kati ya Februari 27 na Machi 3, mwaka huu na kwamba Samson alikuwa wa kwanza kuuawa na kisha mwili wake kutelekezwa porini kisha watuhumiwa wakamuua mkewe na kuutelekeza mwili chumbani.

Aliwataja watuhumiwa wa tukio hilo la kinyama wanaoshikiliwa kuwa ni Mussa Benard (27) ambaye ni mpwa wa marehemu Jaji Mila, Lusekelo Richard (33), mkazi wa Iyela, Enos Kibonike (38, mkazi wa Iganzo na Amos Ndunguru (59), mkazi wa Iyela.

Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa wengine wawili waliotajwa kwa jina moja kuwa ni Godfrey, dereva wa pikipiki anayedaiwa kuwa kabla ya tukio, alimbeba mtuhumiwa namba moja pamoja na Paulo.

Alidai kuwa chanzo cha mauaji hayo ni tamaa za Mussa kutaka kumiliki mali za marehemu Jaji Mila ambazo zilikuwa ndani ya nyumba ambayo ilikuwa inalindwa na Samson na kwamba uwapo wa mlinzi huyo ulikuwa unakwamisha tamaa zake hizo.

"Ninawaomba wananchi mtoe ushirikiano ili na hawa waliotoroka, wakamatwe maana ninyi ndiyo mnaishi nao na mnawafahamu vizuri. Hatuwezi kukubali umaskini wa watu wachache ugharimu maisha ya watu wengine," alisema Kamanda Matei.

Diwani wa Iyela, Mussa Ismail, alisema tukio hilo lilileta taharuki kwa wananchi wake na hivyo akaviomba vyombo vya ulinzi na usalama mkoani humo kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika ili iwe fundisho kwa wengine.

"Ninawaomba wananchi wa Kata ya Iyela kuendelea kuwa watulivu wakati tukisubiri taarifa ya kuwakamata watuhumiwa wote wa mauaji chini ya ushirikiano na Jeshi la Polisi pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama," alisema Ismail.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyefika eneo la tukio kwa ajili ya kutoa pole kwa familia ya marehemu, aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi zaidi wa tukio hilo ili kuwabaini na kuwakamata wahusika wote.

Alisema tukio hilo ni la kinyama, akiwataka vijana kufanya kazi kwa bidii ili wajipatie mali zao kihalali badala ya kutegemea mali za ndugu zao.

Inadaiwa kuwa baada ya kufanya mauaji hayo, Mussa alikwenda kufungua nyumba hiyo na kutaka kusomba mali zilizokuwamo ndipo wananchi wakamshtukia na kutoa taarifa serikalini na ndipo akakamatwa na gari lililokuwa linatumika, likachukuliwa na kupelekwa polisi.

# Ahueni mikopo elimu ya juu yanukia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema serikali inaendelea kufanyia kazi malalamiko kuhusu mfumo wa urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Februari 11 mwaka huu, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliitaka serikali kufanyia kazi malalamiko hayo, akionya kuwa mikopo hiyo imegeuka biashara.

Katika kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo, Nipashe jana ilimtafuta Waziri Ndalichako, ambaye alisema suala hilo linafanyiwa kazi.

"Litakapofanyiwa kazi, tutatoa taarifa," Profesa Ndalichako alisema bila kutaja tarehe ambayo utekelezaji wake utakuwa umekamilika.

**KAULI YA SPIKA**

Katika kikao cha Bunge cha Februari 11, mwaka huu, Spika Ndugai, alisema mikopo inayotolewa na serikali kwa wanafunzi wa elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imegeuka biashara.

Spika Ndugai alisema riba inayodaiwa na HESLB inakuwa mzigo na wanaoumia zaidi ni watoto wa maskini.

Miongoni mwa malalamiko yanayotolewa na wadaiwa ni ongezeko la makato ya mkopo huo kutoka asilimia nane hadi asilimia 15 kwa mwezi kutoka katika mshahara ghafi wa mdaiwa au mnufaika.

Mengine ni tozo ya kutunza thamani ya mkopo ya asilimia sita, tozo ya asilimia moja ya shughuli za kiutawala na adhabu ya asilimia 10 ya deni linalodaiwa kwa anayechelewa kulipa deni baada ya miaka miwili tangu kuhitimu chuo.

"Hii ni kweli maana kumpa mtoto wa masikini mkopo wa elimu halafu unakuja kumdai mkopo na riba, siyo sawa! Hiyo ni sawa na biashara," Spika Ndugai alisema siku hiyo.

Alitahadharisha kuwa utaratibu huo hauendani na kauli ya kuwasaidia wanafunzi na hauna tofauti na wanaokopa fedha za kununua magari.

Kimsingi, kauli hiyo ya Spika Ndugai ilitokana na hoja ya Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM), Ramadhan Ihondo, aliyependekeza riba kuondolewa katika mikopo ya elimu ya juu.

Ihondo alisema serikali haiwasaidii vijana wa Kitanzania katika elimu bali inawakomoa kutokana na riba kubwa inayotozwa.

Miaka miwili iliyopita, Nipashe ilichapisha ripoti kuhusu suala hili, wanufaika wa mikopo hiyo wakilalamika deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka, kunakosababisha ugumu wa kumaliza kulilipa.

Takwimu za HESLB katika kipindi hicho, zilionyesha kati ya Watanzania 479,779 waliopatiwa mikopo hiyo tangu serikali ilipoanza kuitoa mwaka 1994, ni wanufaika 11,214 (asilimia 2.3) waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao.

Kifungu 7.2.1.1 cha Mwongozo wa HESLB wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa Wanafunzi, kinabainisha kuwa mnufaika wa mkopo wa bodi hiyo atalipa tozo ya kulinda thamani ya fedha ambayo itakatwa asilimia sita kwa mwaka tangu tarehe ya mnufaika aliyoanza kupokea mkopo.

Pia katika kifungu 7.2.1.2 cha mwongozo wake huo, HESLB inabainisha itakata asilimia moja ya ada ya uendeshaji kwa mwanafunzi mnufaika.

Vilevile, katika kifungu 7.2.1.3 cha mwongozo huo, inaelezwa kuwa ikiwa mnufaika atashindwa kulipa mkopo baada ya kipindi cha neema cha miezi 24 baada ya kuhitimu masomo yake, ataongezwa makato ya adhabu ya asilimia 10 ya mkopo aliopewa.

# Mgomo mabasi abiria warindima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ABIRIA waliokuwa wanatarajia kusafiri kutoka jijini Mbeya kwenda mikoa ya Kanda ya Ziwa, wamekwama katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mkoa wa Mbeya baada ya mabasi yanayofanya safari zake kati ya jiji hilo na Mwanza kugoma.

Mabasi hayo yalianza mgomo huo jana asubuhi, chanzo kikidaiwa mgogoro uliopo kati ya Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) na serikali kuhusu matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao ulioanzishwa hivi karibuni.

Nipashe ilifika katika Kituo Kikuu cha Mabasi Mbeya majira ya saa 12:15 asubuhi na kukuta mabasi ya kwenda katika mikoa mingine yakiwa yanaendelea kutoka isipokuwa yanayoelekea Mwanza ambako kuna kampuni tatu pekee za mabasi zinazotoa huduma hiyo kwa sasa. Baadhi ya mabasi hayo yalikuwa yameegeshwa kituoni hapo na baadhi yalikuwa hayajulikani yaliko huku abiria wakiendelea kusubiri serikali iwasiliane na wamiliki wa mabasi hayo na baadhi wakaamua kudai warejeshewe nauli zao ili watafute usafiri mwingine.

Meneja wa Kampuni ya Mabasi ya Isamilo Mkoa wa Mbeya, Juma Mohamed, alisema walikuwa tayari kuendelea na safari, lakini walipigiwa simu na wamiliki wakiwaelekeza kutosafirisha abiria. "Kinachosumbua ni tiketi za kielektroniki ambazo serikali inataka tutumie wakati sisi tunataka tutumie za kawaida. Kwa sasa sisi tunasubiri utaratibu kutoka kwa mabosi wetu ambao ndiyo waliotuambia tusiondoe magari," alisema Mohamed.

Mmoja wa abiria waliokutwa stendi jana, Ndamo Jidaha, alisema alikata tiketi juzi kwenye basi la Kampuni ya Premier, lakini jana asubuhi hakukuta basi stendi na alipouliza, aliambiwa halisafiri na akaahidiwa kufaulishwa kwenye gari la Kampuni ya Isamilo.

Alisema alipofika kwenye kampuni hiyo ya Isamilo, alikuta milango imefungwa na abiria hawaruhusiwi kuingia na alipoulizia kilichokuwa kinaendelea, aliambiwa ikishindikana atarudishiwa nauli yake.

"Mimi nimetoka Chunya, nimefika hapa ninakuta usafiri hamna, sasa hivi ninawaza kwamba endapo itashindikana nirudishiwe nauli ili nirudi tena Chunya nikajipange upya?" Alisema Jidaha.

Chama cha Kutetea Abiria nchini (CHAKUA), kimelaani kitendo cha wamiliki wa mabasi hayo kusitisha safari wakati tayari walikuwa wameshachukua fedha za abiria na kuwaacha wakihangaika stendi.

Mjumbe wa Chama hicho, Laudeni Mwambona, aliiomba serikali na TABOA kumaliza mgogoro huo ili kuondoa tatizo kwa wananchi ambao wanapata shida.

Alisema chama hicho kinakubaliana na matumizi ya Tiketi Mtandao kwenye mabasi kwa maelezo kuwa kama taifa ni lazima liendane na mabadiliko ya teknolojia ambayo yanaendelea duniani. Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Denis Daudi, alisema wanaendelea kuwasiliana na wamiliki wa mabasi hayo ili wawajibike kuwasafirisha abiria waliokwama kituoni huku wakiwa wamechukua fedha zao.

Daudi alisema endapo wamiliki wa mabasi hayo wataendelea na mgomo huo, watachukuliwa hatua za kisheria kwa maelezo kuwa mabasi yanayofanya safari kwenda mikoa mingine, yalikuwa yanaendelea na safari zake.

## HABARI KITAIFA

# Waasisi TAMWA wapewa tuzo

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimetoa tuzo za heshima za kutambua mchango wa waasisi wake 12 katika kuadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk. Harrison Mwakyembe, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika jana, jijini Dar es Salaam, aliwapongeza TAMWA kwa kutambua na kuenzi mchango mkubwa wa wanawake 12 walianzisha chama hicho katika wakati ambao dunia ilikuwa imetawaliwa na mfumo dume.

Dk. Mwakyembe alisema ameshuhudia mafanikio makubwa ya TAMWA yaliyofikiwa kwa juhudi za waasisi hao, ikiwamo kusaidia kupunguza matukio ya ukatili yaliyokuwa yakiliitia aibu Taifa kama mauaji ya watu wenye ualbino.

Alisema wakati huo waasisi walifanya mapambano ya kupinga masuala ya ukatili hali haikuwa rahisi na kauli iliyokuwa ikitawala ni kuwa kila mwanaume mwenye mafanikio nyuma yake kuna mwanamke.

"Ikaja tena na kauli ya mwanamke akiwezeshwa anaweza ilipokelewa tena kwa nguvu na kufanya wanawake kutembea kifua mbele," alisema Dk. Mwakyembe.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, alisema waliamua kuadhimisha Siku ya Mwanamke kwa kuwaenzi waasisi hao 12 ambao walikuwa na msukumo wa kutetea haki za wanawake na watoto wa kike.

Aliwataja wanawake hao aliowaita malkia wa nguvu kuwa ni Halima Shariff, Elizabeth Marealle, Rose Kalemera, Leila Sheikh, Nelle Kidela (marehemu) Fatma Alloo, Edda Sanga, Ananilea Nkya, Rose Haji, Pili Mtambalike, Jamila Chipo (marehemu) na Valirie Msoka.

"Bila waasisi hawa, haya yote yasingefanyika. Tunathamini maamuzi yao, shughuli za kukiunda, kukikarabati na kisha kukiweka chombo hiki majini, hadi sasa kinapoelea kwa fahari," Reuben.

Alisema kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema 'Mwanamke katika uongozi, chachu kufikia dunia yenye usawa' wanajivunia waasisi hao wa TAMWA ambao wameweza kutimiza wajibu wao.

Aidha, aliwataka wanawake vijana kuanzisha mawazo yatayosaidia watu wengine kama ambavyo waasisi hao walivyofanya.

"Waasisi walionzisha TAMWA wawili kati yao wameshafariki dunia, lakini mawazo yao yanaishi hadi sasa, haki zinatendeka chini ya sheria zilizopitisha kupitia mawazo waliyoyatoa. Niwaase wanawake vijana msilale na mawazo yawasilisheni kwa ajili ya kusaidia mabadiliko ya wenzetu," alisema Reuben.

Naye Mwasisi wa TAMWA, Rose Haji alisema haikuwa kazi rahisi kuanzisha TAMWA wakati huo, changamoto zilizokuwa nyingi, lakini walishikamana kuhakikisha wanatimiza lengo hilo katika wakati ambao wanawake walikuwa hawapewi kipaumbele kwa kuwa hawakuaminika.

Naye Mwasisi Fatma Alloo, mbali na kuelezea harakati za kuanzisha TAMWA na mapambano ya kutetea haki za wanawake na watoto, aliwaasa wanahabari wake kupendana, kufanya kazi kwa bidii, kutimiza malengo waliyojiwekea na kujiendeleza kimasomo na kusoma vitabu mbalimbali.

# Ubomoaji nyumba 100 za Dar wachukua sura mpya

**Na Romana Mallya**

UBOMOAJI wa nyumba takribani 120 katika eneo la Mabibo Kisiwani wilayani Ubungo mkoani Dar es Salaam, umechukua sura mpya baada ya serikali kuelekeza viongozi wa eneo hilo kukata rufani.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam, Idrisa Kayera, alisema baada ya tatizo hilo kutokea, wametoa maelekezo kwa viongozi wa eneo hilo kuwataka wakate rufani mahakamani.

"Kimsingi hakuna kitu kipya ila muhimu tushirikiane na wananchi kwa maana kwamba wanatakiwa kutekeleza majukumu fulani fulani, kwa sababu kitu kikiamuliwa na mahakama ni mahakama tu inaweza kubadilisha uamuzi, tunachofanya tunaendelea kushauri wafanyeje ili kuhakikisha suala linapungua.

"Moja ya mambo tumewaambia wahakikishe ni kukata rufani leo (jana) na kupata zuio la mahakama, tumeshawaambia na kuwapa mwelekezo. "Ni kwa sababu mahakama ikishasema mtu fulani amefungwa, huwezi kutumia nguvu kumtoa. Unachotakiwa ni kutazama fursa sehemu gani unaweza kupita ili kuhakikisha suala hilo linakwisha. Njia pekee na ya haraka ni kupata zuio la mahakama na rufani," alisema.

Kamishna Kayera alisema mwenyekiti wa kamati wa eneo hilo anafuatilia kuhakikisha wanapata vitu vinavyohitajika ili kukata rufani.

"Ninavyoona siyo suala kubwa, linaweza kuisha kwa maana kwa kupita njia zilezile za mahakamani ili kuweza kulimaliza," alisema.

Juzi, Nipashe iliripoti kuhusu uwezekano wa kubomolewa kwa nyumba hizo ifikapo Jumanne ijayo kutokana na kuwapo kwa amri ya mahakama.



Aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kulia), akimkabidhi tuzo mmoja wa waasisi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Fatma Allo (kushoto), wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa kuwaenzi waanzilishi wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Wapili kulia ni Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe na Mkurugenzi wa chama hicho, Rose Reuben. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri akerwa madereva kutopewa mikataba kazini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amekerwa na kitendo cha waajiri nchini kuendelea kuwatumia madereva kufanya kazi bila kuwa na mikataba rasmi.

Mhagama aliweka wazi kukerwa na kitendo hicho wakati wa kikao cha majadiliano kuhusu kero za madereva katika sekta ya usafirishaji nchini.

Kikao hicho kilihusisha Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri nchini pamoja na wadau mbalimbali katika sekta ya usafirishaji.

Alisema sekta hiyo ni moja ya maeneo ambayo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi, hivyo wadau walipo, wanatakiwa kutimiza wajibu wao ipasavyo. Waziri huyo alisema sekta ya usafirishaji isipokuwa na utulivu, uchumi wa nchi hautakuwa kwa kuwa madereva ndiyo wanahusika katika usafirishaji bidhaa na wafanyabiashara.

"Ninashindwa kuelewa kwanini madereva hadi leo hii wanaendelea kufanya kazi bila ya kuwa na mikataba pamoja na hatua ambazo tumekuwa tukichukua.

"Sasa, ninaagiza baada ya kikao hiki, kiitishwe kingine ambacho kitawahusisha waajiri ili tufikie makubalianao," Mhagama aliagiza.

Alisema kuwa baada ya kufanyika kwa kikao hicho, makubaliano yatakayofikiwa ndiyo yatatumika kuchukua hatua kwa yeyote atakayekwenda kinyume.

"Lazima tujadiliane na kubaini nani mwenye shida. Kama ni madereva au waajiri ndiyo wenye shida na kufanya makubalinao na baada ya hapo tutaanza kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria na miongozo mbalimbali ya nchi na mikataba tuliyosaini kimataifa," alionya.

Vilevile, aliwataka waajiri kuacha kutumia nafasi zao kuwanyima haki wafanyakazi kuanzisha vyama vyao.

"Uoga wa waajiri juu ya vyama hivi sasa hauna maana kwani hivi vyama vya wafanyakazi vinatumika kama daraja baina ya waajiri na wafanyakazi, hivyo hakuna sababu ya kuvihofia," alisema.

Aliwataka waajiri pamoja na wafanyakazi kuwa na utaratibu wa kukaa meza moja kujadiliana kero mbalimbali ili kuzuia kwa migogoro katika maeneo ya kazi.

Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri nchini, Pendo Berege, alisema lengo la kikao hicho ni kujadiliana kero zilizopo kwenye sekta ya usafirishaji hususani madereva ili zipatiwe ufumbuzi.


**GSP AUCTION MART**

P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. AFCL/2021/DM/020**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Ijumaa tarehe 26/03/2021 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP909 BUS | T351DPS | DAR ES SALAAM |
| HEKIMA GERVAS BIDYANGUZE | LPO 909 | T421DRX | DAR ES SALAAM |
| HEKIMA GERVAS BIDYANGUZE | LPO 909 | T763DRX | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613DMQ | DAR ES SALAAM |
| FRED MALIN KAZI | XENON | T449DTV | ARUSHA |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

# Halotel yasaidia mil. 5/- watoto wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha kulelea watoto wenye ulemavu wa mfumo wa ufahamu, Salt Vocational Training Center cha Makabe, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, kimepewa msaada wa Sh. milioni tano na Kampuni ya Halotel, kuunga mkono juhudi za wanawake wapambanaji kusaidia kuleta mabadiliko kiuchumi.

Kituo hicho kinachoongozwa na mwanamke kinatoa elimu ya ujuzi na ufundi stadi kwa watoto licha ya changamoto za ufahamu wanazokabiliana nazo.

Katika mwendelezo wa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Kampuni ya Halotel Tanzania imetoa msaada huo kuunga mkono juhudi za wanawake wapambanaji katika majukumu yao ya kuleta mabadiliko chanya katika nyanja mbalimbali ikiwamo kiuchumi, kijamii na kujenga taifa.

Kiongozi wa kituo hicho, Rebeka Lebi, alisema kituo chake kina watoto zaidi ya 22 wanaokabiliwa na tatizo la mfumo wa fahamu ikiwamo usonji, udumavu, mtindio wa ubongo na kifafa. "Kutokana na changamoto hizi na wazazi kukosa kipato cha kuwasaidia, wanashindwa kupata msaada wa malezi ya karibu," alisema.

Akitoa msaada huo, Ofisa wa Habari Halotel, Hindu Kanyamala, alisema Halotel inajisikia furaha kuendelea kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani na Rebeka kwa kutambua na kuunga mkono juhudi zake za kulea watoto hao.

"Tunampongeza kwa kuona umuhimu wa kulea na kutoa ujuzi kwa watoto hawa na kuleta mtazamo na matokeo chanya kwa jamii kwa ujumla. Hivyo kiasi hiki tulichokitoa tuna imani kitasaidia watoto hawa kusogea mbele zaidi," alisema.

Kwa upande wake kiongozi wa kituo hicho, Rebeka alisema; "Tunashukuru sana uongozi wa kampuni ya Halotel kwa kutambua umuhimu wa kituo hiki na kile tunachokifanya, msaada huu umekuja kwa muda muafaka na utatusaidia katika ununuzi wa vifaa vya kufundishia na mahitaji mengine, hapa kituoni. Watoto hawa wamekuwa wakikumbwa na changamoto mbalimbali za kimalezi wanapokuwa majumbani, wengine wamekuwa wakipitia changamoto za unyanyasaji wa kijinsia na kutopata malezi bora, tukaona kupitia sisi Salt Center tunaweza badilisha maisha ya watoto hawa kwa kuwapa ujuzi ili waweze kuwa chachu na waweze kujitegemea na kushiriki katika ujenzi wa taifa."




Mkuu wa Kitengo cha Idara ya Masoko Halotel, Sakina Makabu, akikabidhi msaada wa Sh. 5,000,000 kwa Mkuu wa kituo cha kulea na kutoa mafunzo na ufundi stadi kwa watoto wenye changamoto ya ulemavu wa mfumo wa fahamu Rebeka Lebi. Kushoto ni Ofisa Mawasiliano, Hindu Kanyamala na Stella Pius. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule maalum watoto wenye ulemavu yapokea wanafunzi

**Na Augusta Njoji,** ARUSHA

HATIMAYE shule maalum ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya Patandi iliyoko Arusha, imeanza kupokea wanafunzi baada ya serikali kukamilisha ujenzi wake kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R).

Ujenzi wa shule hiyo umegharimu Sh. bilioni 3.6 na ni shule ya kwanza ya serikali nchini kujengwa kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Akizungumza jana na Nipashe, Mkuu wa Shule hiyo, Janeth Mollel, alisema hadi sasa wanafunzi 143 ambao kati yao 93 ni wenye ulemavu, wameripoti kuanza masomo wiki mbili zilizopita.

"Hii shule inachukua watoto hawa wenye mahitaji maalum nchi nzima. Tunashukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga shule hii ambayo ni ya kipekee Tanzania nzima na inawezekana pia Afrika Mashariki," alisema.

Mollel alisema shule hiyo upekee wake inachukua wanafunzi wa aina zote wa elimu jumuishi na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi wa bweni na kutwa 600 huku uwezo wake wa mabweni ni kuchukua wanafunzi wa 416.

"Kuna watoto wenye ulemavu wa aina zote wanasoma hapa. Watoto wasiosikia na wanaotumia viti mwendo, miundombinu ya shule hii imezingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu. Kuna vyumba maalum kwa ajili ya wanafunzi ambao wana ulemavu mkubwa wa viungo na vyumba hivyo vina vyoo ndani," alisema.

"Education for Efficiency"

TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY

TIA

**TAASISI YA UHASIBU TANZANIA (TIA)**

**KURASINI, MAKUTANO YA BARABARA YA KILWA/NELSON MANDELA**
**Barua zote zijibiwe kwa**
**Afisa Mtendaji Mkuu – TIA**
**Simu Na. 02850717**
**Nukushi.: 0736502630**
**Barua pepe: tia@tia.ac.tz**
**Tovuti: www.tia.ac.tz**

**S. L. P. 9522,**
**DAR ES SALAAM,**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MADAI YA MWANAFUNZI WA TIA KUTIWA MBARONI KWA TUHUMA ZA MADAWA YA KULEVYA**

**Dar es Salaam, Jumatano Machi 10, 2021.**

Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) **inakanusha taarifa** iliyoandikwa na Gazeti la Mwananchi toleo la Jumatano, Machi 10, 2021, ukurasa wa 1 zenye kichwa cha habari **"Mwanafunzi TIA mbaroni kwa 'unga'".**

Kama ilivyonukuliwa na gazeti hilo, mtuhumiwa Bi. Allu Murugwa (24) alidahiliwa na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) na kusajiriwa kwa namba DSM/DBA/18/51801, katika kozi ya Stashahada ya Usimamizi wa Biashara. Bi. Allu Murugwa alihitimu mafunzo yake mwaka 2020, hivyo, **kwa sasa siyo mwanachuo wa TIA.**

Kwa taarifa hii, Umma unafahamishwa kwamba, tuhuma zinazomkabili Bi. Allu Murugwa, hazina uhusiano wowote na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA).

Imetolewa na;

*Lillian Mpanju Rugaitika*
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano**

# Z'bar yatoa msimamo chanjo corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema wizara yake haitakubali chanjo ya corona, mpaka madaktari wakae pamoja na kufanyia uchunguzi ubora wa chanjo hiyo.

Amesema iwapo wataridhika na ubora wake, watakuwa tayari kutumia ikiwa maradhi hayo yataendelea kuwapo nchini.

Mazrui aliyasema hayo jana baada ya Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Andermichael Ghirimry, kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kutoa takwimu za wagonjwa wa corona ili kulisaidia shirika hilo kupata takwimu sahihi za maambukizi mapya na vifo vinavyosababishwa na maradhi hayo.

Mwakilishi huyo wa WHO alitoa ombi hilo katika ofisi ya wizara, Mnazi Mmoja, baada ya kuwasilisha ripoti ya mpango mkakati wa WHO ya kutokomeza maradhi ya kipindupindu Zanzibar.

Dk. Ghirimry alisema kuna changamoto ya kupata takwimu za wagonjwa na vifo vinavyotokana na corona, hivyo kutokujua hali ya tathmini ya maradhi hayo.

Pamoja na kuweka msimamo huo, Mazrui aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maradhi ya corona na kwamba bado maradhi hayo yapo duniani. Alisema kutokana na uwapo wa ugonjwa huo, ni wajibu wa kila mwananchi kuchukua tahadhari na kuepuka misongamano isiyo ya lazima pamoja na kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya kujikinga na maradhi hayo ambayo yamegharimu maisha ya watu wengi duniani.

"Maradhi ya kupumua ambayo kwa sasa yanawapata Watanzania si corona na kuna baadhi ya wagonjwa hupata maradhi ya kupumua wakipimwa hawana corona na wengine hukutwa na maambukizi ya corona bila kuugua maradhi ya kupumua," alisema.

# MATANGAZO

IITA Transforming African Agriculture — IRRI

## POSITION ANNOUNCEMENT

### Researcher
### IITA-TZ-2021 - IRRI-004 -NRS- DAKAWA -MOROGORO

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of Researcher.

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium. IRRI develops and promotes new rice technologies such as high yielding varieties, climate and stress resilient varieties and technologies that offer the promise of increased productivity with optimum resources and hence ensure the welfare of farmers.

**Duty Station:** The position will be based Dakawa - Morogoro, Tanzania.
Criteria for Success / Qualifications
- Bachelor of Science Degree in Agriculture
- Minimum 2 years of relevant work experience in plant breeding

**Skills and knowledge**
- Familiarity with quality control tools
- Proven technical proficiency in conducting research experiments preferably in the field
- Strong analytical skills
- Strong oral and written communication skills
- Strong organizational and interpersonal skills

**Responsibilities**
1. Plan the implementation of routine experiment(s) in the field of Plant Breeding to support projects goals of the Organizational Unit's (OU's) research objectives related to breeding
   - Coordinate with collaborators on their research activities as required
   - Plan the support/manpower needed and set up work schedule
   - Prepare the material and equipment needed based on research outline provided
   - Assist in applying methods/techniques that guarantee the success of the experiments
2. Assist in supervising the implementation of experiments in the field of Plant Breeding
   - Oversee the work of research technician and/or contract workers to ensure that research activities are implemented according to plan and specific standards
   - Coordinate with collaborating OUs the timely supply of material needed
   - Contribute to the preservation of research areas and direct the maintenance of technical equipment (repair and replacement)
3. Collect and analyze research data in the field of Plant Breeding
   - Collect and process data to its required form
   - Identify inconsistencies in the data collection and/or missing information
   - Carry out graphical and basic statistical data analysis
   - Update database for storage and retrieval of information/data
4. Contribute to the preparation of reports and publications, and presentations in the field of Plant Breeding
   - Provide appropriate data and information about experiment(s)
   - Contribute to manuscripts/write —ups for annual reports and publications in referred journals as well as
   - presentation/posters for national and international conference
5. Support the training of scholars, partners and on-the-job trainees as required
   Act as resource person for training courses and visitors

6. People Management
   - Supervise the work of Research Technicians
   - Provide feedback on performance of Research Technician to immediate supervisor
   - Assist Students and Trainees

7 Perform any other duties as assigned by Supervisor from time to time

**General information:**
The duration of contract for the position is two years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:**
Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.
**Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

IITA Transforming African Agriculture — IRRI

## POSITION ANNOUNCEMENT

### Seed Systems Specialist
### IITA-TZ-2021 - IRRI-003 -NRS-MOROGORO

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of Seed Systems Specialist

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium. IRRI develops and promotes new rice technologies such as high yielding varieties, climate and stress resilient varieties and technologies that offer the promise of increased productivity with optimum resources and hence ensure the welfare of farmers. There is a need to scale up the adoption of these varieties /technologies for faster impacts. Farmer-to farmer exchange of seeds is considered to be the main mechanism for the widespread dissemination of varieties. The dimension of farming system has changed in terms of the preference of the farmers, use of mechanized agriculture, men moving out for work and women holding the charge for farming. It's important to conduct research that can suggest interventions for awareness creation, demand creation, adoption and impact of new varieties. It is also important to compare and find the pros and cons of different delivery/extension approaches for dissemination of these varieties.

Under the supervision of Seed Systems and Product Management Lead - Africa , the Seed Systems specialist will work around, strengthening seed systems and extension research, promoting rural innovation, partnership and liaisoning, monitoring and evaluation of seed systems' development. Monitor the strategic collaboration around seed systems and extension research, conceptualize, design and execute research with the aim of evaluating the ongoing seed systems activities across different key projects in Tanzania and strengthen the same; and interact cohesively with the regional team in relevant activities.

**Duty Station:** The position will be based Morogoro, Tanzania.
**Criteria for Success / Qualifications**
- Bachelor's degree in Agriculture/ Agri business/Rural development with minimum 4 years of relevant work experience around agriculture extension, rural livelihoods, sustainable agriculture/development and project management.
- Master's degree in Agriculture/ Agri business/Rural development with minimum 2 years of relevant work experience around agriculture extension, rural livelihoods, sustainable agriculture/development and project management.

**Skills and knowledge**
**mandatory**
- Knowledge and extensive experience in the field of agriculture extension, agri-business planning, rural development
- Strong oral and written communication skills and scientific documentary skills
- Strong organization and interpersonal skills
- Experience of working with government stakeholders (Ministries, nationals partners)
- Experience of extensively working with and managing partners
- Experience with gender and rural development approaches
- Experience on data analysis and relevant statistical tools

**Preferred**
- Working experience in stakeholder management, development research, and applied agri-economics
- Work experience with international organizations
- Good understanding of rural livelihood systems

**Responsibilities**
**3.1. Purpose**
- Monitor and manage the strategic collaboration around seed systems and extension research. Conceptualize, design, execute collaborative research to evaluate and improve good quality seed demand creation approaches across various regions in Tanzania
- Promote, manage various rural development and innovation models around extension/seed systems/climate smart technologies engaging various institutions, change agents and stakeholders
- Identify gender- and market-responsive seed systems interventions and extension approaches for enhancing livelihoods, including demonstration of new varieties to generate demand and capacity building of local institutions
- Recommend approaches for promoting seed entrepreneurship amongst women and youth and their collectives
- Design, manage and monitor research activities including necessary protocols, research tools, data collection, analysis and interpretation

Establish and promote strategic partnership, innovation forums and partner management for key projects

**3.2. Engagement**
- Consult and collaborate with NARES/ Govt and non-Govt extension agencies, and private sector partners for strengthening seed systems and extension research and new approaches in seed and delivery systems
- Work closely with partners, facilitators, enumerators for executing surveys and various research-oriented interventions
- Collaborate with NGOs, Community based institutions, women's groups for innovation in extension approaches, gender-responsive interventions and piloting seed entrepreneurship models
- Engage with knowledge agencies, training institutions and experts for stakeholder capacity building and strengthening partnership
- Monitor and manage field technical staff for strengthening outreach programs, monitoring, evaluation, action research and experiments

**3.3. Delivery**
- Research studies designed, managed, analyzed and interpreted
- Documentation of research findings including data collection, analyses and reporting, measured outcomes, impacts
- Technical literature and publication in scientific journals/websites
- Knowledge and communication products including website, blogs, newsletters, etc
- Various extension models and interventions for farmers, women farmers and key stakeholders executed, monitored and evaluated
- Contribute to the development of concept notes and projects for funding or technical collaborations for research and development jointly with relevant IRRI staff
- Develop and contribute towards documentary outputs like knowledge products and research document/ publications/scientific writing/policy briefs

***General information:***
The duration of contract for the position is two years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date
of advertisement appearing in the newspaper.
**Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kurasimisha makazi, kupima ardhi utakuwa mwarobaini migogoro

**WIZARA** ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inahamasisha urasimishaji wa makazi na kupima ardhi, kwa kuweka utaratibu maalum ambao unawezesha kila kipande cha ardhi kupimwa na kuwa na kumbukumbu muhimu zinazotuzwa kianalojia na digitali.

Katika baadhi ya maeneo kazi ya urasimishaji imepewa kampuni, ambazo baadhi zimefanikiwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo, lakini katika maeneo mengine kazi haijafanyika.

Kurasimisha makazi kunawezesha kuwa na taarifa sahihi za umiliki wa ardhi, kuongeza thamani ya ardhi, mapato kwa kuwa sasa serikali itajua idadi ya wamiliki na kiasi cha kodi wanayotakiwa kulipa kila mwaka.

Lakini kwa upande wa ardhi ambayo haijaendelezwa ikipimwa, itaongezeka thamani kwa kuwa mmiliki atakuwa na hatimiliki ambayo ni nyaraka muhimu anayoweza kuitumia kwenye taasisi za fedha kuomba mkopo.

Kuchelewa urasimishaji wa ardhi ni kuchelewesha maendeleo na kuendeleza migogoro ya ardhi, ambayo siyo lazima kwa kuwa kila kipande cha ardhi kikishakuwa na mmiliki anayetambulika, maana yake siyo rahisi mtu kuvamia.

Wiki iliyopita, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, aliagiza kuchukuliwa hatua watendaji wote wa Chuo cha Ardhi Morogoro waliochelewesha urasimishaji makazi katika Kata ya Kivule, Dar es Salaam.

Hii ni sehemu moja kati ya nyingi zinazotakiwa kurasimishwa, lakini kwa sababu mbalimbali hakuna utekelezaji, jambo ambalo linachelewesha nia thabiti ya kushughulikia migogoro ya ardhi.

Mathalani, Machi 15, mwaka huu, utekelezaji wa amri ya Mahakama kubomoa nyumba za watu eneo la Tabata Kisimani Manispaa jijini Dar es Salaam utaanza, na kaya zaidi ya 100 zitaathirika ambazo zinadaiwa kujenga eneo la viwanda.

Dar es Salaam ina mpango mkuu wa ardhi wa miaka ya 70 ambao mara kadhaa imefanyiwa mapitio, lakini kumekuwa na uvamizi kwa kuwa yapo maeneo yahajaendelezwa kwa muda mrefu na wananchi walipoanza kujenga hawakuchukuliwa hatua, huku wengine wakimilikishwa kisheria.


Katika maeneo mengi ya miji bado urasimishaji wa ardhi na kuwapo kwenye mfumo wa kidigitali haujafanyika na ndiyo maana miaka 60 ya Uhuru bado migogoro ya ardhi inashika kasi, na utapeli mwingi unafanyika kwenye ardhi.

Katika kata kuna kamati za ardhi ambazo moja ya majukumu yake makuu ni kusimamia ardhi ya eneo husika na kuhakikisha taratibu zinafuatwa, lakini kwa maeneo mengi kinachofanyika ni kukusanya fedha za asilimia 10 ya mauzo ya ardhi, huku mchezo wa kumilikisha ardhi husika ukiendelea.


Ni muhimu sana wizara na mamlaka za serikali za mitaa zikatoa elimu sahihi kwa wananchi, ili wajue hatua za kufuata hadi makazi yake yarasimishwe au umiliki ardhi, kwa kuwa wengi hawafahamu na ndipo matapeli hupata nafasi ya kutenda ubaya.

Iwapo nchi itafanikisha urasimishaji wa ardhi, ni wazi itakuwa rahisi kutekeleza mpango bora wa maendeleo ya ardhi kwa kutenga ardhi kulingana na matumizi, jambo ambalo litapunguza kama siyo kumaliza migogoro kati ya wakulima na wafugaji, mtu na mtu, taasisi na mtu, taasisi na taasisi, hifadhi na binadamu pamoja na wanyamapori na binadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Tutambue kwanza mfumo dume unawaumiza wahitaji, wajane

**MFUMO** dume ni matokeo ya dhana za kurithi, imani za kidini, mila na utamaduni ambazo zinamkandamiza mwanamke na mtoto wa kike.

Katika kuhakikisha wanawake na mabinti zao wanapata haki za msingi, kunatakiwa suala la mfumo dume lisiwepo kwa kunyimwa nafasi.

Kama bado kutakuwapo familia zinazoendekeza mambo ya mfumo dume, wajue wanaendelea kuwanyima haki wanawake na watoto wa kike.

Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, kilele chake kilikuwa Jumatatu wiki hii, ilianikwa namna mfumo dume umekuwa sababu ya kudidimiza haki za wajane kwa baadhi ya jamii.

Mojawapo ni kutoka kwa Ally Mzava, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mnadani, Kata ya Majohe, katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, alipoadhimisha siku hiyo maalum kwa kinamama katika viwanja vya Kipunguni, ndani ya eneo lake.

Mwenyewe alikuwa na ufafanuzi niliyoupenda kwa nukuu hii: "Elimu inatakiwa itolewe, ili wanawake wazitambue haki zao na kama hakutakuwa na elimu, baadhi ya wanawake wajane wataendelea kupoteza haki zao."

Mzava, pia anasema wanawake wanachangia mengi katika maendeleo kitaifa, hata kimantiki mafanikio ya mwanaume nyuma yake yamesimamiwa na mwanamama.

Katika hilo nahimiza kwamba, kuna haja kubwa ya wanaume kuwatambua wanawake, kutokana na namna jinsia hiyo inavyotumia njia salama kulinda mali zao za pamoja.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Amani katika kata hiyo ya Kipunguni, Daniel Malaghashimba, anasema kuwa na wanawake katika safu ya uongozi, ni chachu muhimu ya kufikia dunia yenye usawa wa jamii.

Pia Malaghashimba ana maono kwamba kila panapoadhimishwa Siku ya Wanawake Duniani, ni muhimu na lazima haki za wanawake zilindwe kwa uhalisia wa matendo, akikapatiwa fursa zote muhimu za kazi, kama alivyo mwanaume kwa kadri itakavyowezekana.

"Mwanamke anayo haki ya kupata huduma bora, ikiwamo afya ya uzazi salama na uwezo wa kumiliki mali," anasema.

Hata mdau mwanaharakati kutoka asasi ya kupigania haki za kijamii na kijinsia TGNP Mtandao, Alfonsina Amblosi, anasema kinamama wanatakiwa kuwaelimisha watoto namna ya kuzifahamu haki zao za msingi, ili wanufaike na majina yao ya kila siku, sasa na waendako.

Mdau huyo mwanaharakati, katika mantiki hiyo anahimiza kipaumbele katika haki tatu kuu za mtoto anazozitaja kuwa ni kuishi, kupendwa na kupatiwa elimu.

Anasema wazazi katika nafasi yao nao wanatakiwa kuwazoesha watoto kwa kuwapongeza pale wanapofanya vizuri katika masomo na mambo mengine ya msingi kwao.

"Mtoto ajengewe mambo mazuri na kumnunulia vitu ambavyo una uwezo navyo, ili aweze kuvizoea," anasema.

Alfonsia anasema watoto katika nafasi yao hiyo, wadau hao wa familia - watoto, pia wanapaswa kulelewa katika misingi inayofaa ili wanapofikia umri wa ukubwani, wasije wakabadilika kitabia, bali wabaki katika mkondo unaofaa.

Akizungumzia Siku ya Wanawake Duniani, anawataja wanawake kuwa ni taifa kubwa na pale wanapowezeshwa, daima huwa wanaweza.

Siku ya Wanawake je? Pia hapo ana lake jambo, akisema wanawake wanatumika kuleta maendeleo, hata kama mwanaume akiishi bila mwanamke, bado hawezi kufanya bajeti ya kipato chake kukidhi mahitaji, mwanamke ana nafasi kuwezesha maendeleo yake na huwa yanaonekana.

HABARI KITAIFA

# Walimu 100 kunolewa Kifaransa

**Na Salome Kitomari**

MABALOZI wa nchi zinazozungumza Kifaransa nchini, wamesema lugha hiyo inazidi kukua Tanzania na kwa kushirikiana na serikali imeandaa programu maalum ya kufundisha walimu 50 hadi 100 wa lugha hiyo kila mwaka.

Wakizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kifaransa, mabalozi wa nchi zinazozungumza lugha hiyo zenye ubalozi nchini, walisema lugha hiyo inazidi kukua na jitihada zinafanyika kuendelea kuzalisha wataalamu wengi watakaofundisha Watanzania.

Maadhimisho ya siku hiyo yataambatana na maonyesha ya shughuli mbalimbali za kila nchi kuanzia Machi 17 hadi 31, mwaka huu. Balozi wa Morocco nchini, Abdelilah Benryane, alisema Kifaransa ni lugha ya tano kwa kuzungumzwa duniani na ikiwa ya kwanza na pekee inawakilisha kitaasisi katika nchi za Afrika, Ulaya, Marekani na Asia.

Alisema lugha hiyo inatumika katika nyanja za maendeleo, utamaduni, haki, usawa, demokrasia na haki za binadamu, uchumi, elimu, sayansi na utafiti, na pia kwenye michezo mbalimbali.

Naye Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema kwa kushirikiana na serikali wamekuja na programu ya kufundisha walimu ambao watakwenda kufundisha Kifaransa, kila mwaka watawafikia kati ya 50 hadi 100 huku lengo likiwa ni kufikia 1,000 baada ya miaka 10.

Alisema inakadiriwa kuwa Watanzania milioni 1.5 wanazungumza lugha ya Kifaransa, ikiwa ni lugha pekee ya kigeni baada ya Kiingereza kinachotumika kwenye mitaala ya kufundishia.

# Mkurugenzi shule maarufu Dar ahojiwa na TAKUKURU

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imemhoji Mkurugenzi wa Taasisi ya Munazzamat Dawa Al Islamiya (MDI), Ally Magoga, kwa madai ya kutowalipa mishahara na posho walimu na wafanyakazi wa Shule ya Wasichana ya Kiislamu ya Kunduchi, Dar es Salaam.

Aidha, TAKUKURU inafanyia uchunguzi malalamiko dhidi ya viongozi wa Taasisi ya MDI, inayomiliki baadhi ya shule nchini, ikiwamo ya Wasichana Kunduchi yaliyowasilishwa na baadhi ya walimu na wafanyakazi.

Malalamiko hayo yalitolewa hivi karibuni na baadhi ya wazazi na wanafunzi wa shule hiyo, yalirushwa katika kituo kimoja cha luninga yakiulalamikia uongozi wa shule hiyo kwamba pamoja na mambo mengine, imekuwa ikishindwa kuwalipa mishahara na posho zingine, walimu na wafanyakazi.

Taarifa iliyotolewa na Ofisa Uhusiano wa TAKUKURU, Dorren Kapwani, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, inaonyesha kuwa viongozi wa shule, wanalalamikiwa kusababisha madeni kwa walimu na wafanyakazi.

Inadaiwa kwamba hadi kufikia Machi, mwaka huu, walimu na wafanyakazi wa Shule ya Wasichana ya Sekondari ya Kiislamu Kunduchi wanaidai Taasisi ya MDI Sh. milioni 406 ambayo Mkurugenzi wake hajataka kuwalipa.

Taarifa hiyo ilionyesha kuwa baadhi ya tuhuma zinaangukia chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007.

"TAKUKURU inaendelea kuwahoji walalamikiwa kukusanya vigezo," alisema Kapwani kupitia taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo inaonyesha kwamba Mkurugenzi wa MDI akishirikiana na Mkurugenzi mpya wa Elimu wa Shule ya Kunduchi wamekuwa wakiingia mikataba mibovu ya kuikodisha shule hiyo kwa wamiliki mbalimbali bila kufuata utaratibu.

Malalamiko mengine ni uongozi wa MDI kukwepa kulipa kodi halali za serikali na hivyo kuisababishia serikali hasara na kwamba mapato ya shule yamekuwa yakiishia mikononi mwa wajanja wachache ndani ya taasisi hiyo.

Malalamiko mengine ni kwamba viongozi wa MDI wametangaza kuwaondoa kazini walimu na wafanyakazi wote wa Shule ya Kiislamu ya Kunduchi bila kuwapa malipo yao kwa madai kuwa hiyo ni amri kutoka katika uongozi wa mkoa.

Pia inadaiwa kuwa tangu mwaka 2017 kuna Bodi ya Wadhamini inayoongoza shule hiyo, lakini haijasajiliwa katika Walaka wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu, akimkabidhi cheti na Tuzo Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB, Abella Tarimo, baada ya benki hiyo kuwa mdhamini wa maonyesho ya biashara ya wiki ya wanawake. **MPIGAPICHA WETU**

# Walimu wafundwa kutokuweka ATM rehani mikopo

**Na Augusta Njoji,** ARUSHA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewataka walimu kujiepusha kuweka rehani kadi zao za benki (ATM), wanapokopa fedha kwenye taasisi za fedha.

Aidha, imeagiza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kufukuzwa kazi mwalimu yeyote atakayebainika kuwa mlevi na mtoro kazini.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na walimu na watumishi wa Shule ya Sekondari Ilboru, jijini hapa.

"Mara nyingi nilikuwa nikitembea kwenye halmashauri nasikia kuna tatizo la walimu wanakopa hadi wanaacha kadi za ATM. Najua hapa hawapo, eti kuna wale wa kuacha ATM kadi hapa? Tukisema tuweke mezani zipo?" Alihoji.

"Nashukuru nilipofika hapa Ilboru nimeambiwa walimu wote wana ATM si kama wale wa maeneo mengine kule wanapokopa, niwapongeze sana," aliongeza.

Kuhusu ulevi na utoro, Mweli alisema kuna baadhi ya maeneo nchini aliyotembelea amekuta tatizo la ulevi na utoro kwa walimu ikiwamo Arusha.

"Hata hapa Arusha kuna tatizo la ulevi na kutohudhuria kazini. TAMISEMI tumetoa maelekezo ya jumla kuwa akigundulika mwalimu mwenye tatizo hilo, achukuliwe hatua za kinidhamu ikiwamo kufukuzwa kazi," alisema.

Aidha, alipongeza shule hiyo kufanya vizuri kwenye mitihani ya taifa na kuwataka kuimarisha kusoma kwa vitendo ili kuwaandaa wataalamu wanaoendana na mahitaji ya soko.

"Kuna watu wanasema shule ya Ilboru inafaulisha kutokana na kupeleka watoto wazuri, lakini niseme shule za kata zinapelekewa watoto wazuri zaidi, maana hizi shule za vipaji zinachukuwa wale walioongoza kwenye halmashauri," alisema.

Hata hivyo, alisema tatizo si mtaala wa kufundishia bali ni namna ya kuifundisha na kuwataka wasiishie kuangalia kupata ufaulu wa daraja A wahakikishe wanajifunza kwa vitendo.

"Sekta ya elimu tumepewa kazi moja ya kuandaa nguvu kazi kwa ajili ya sekta nyingine tusipofanya vizuri tujue tumeua sekta nyingine," alisema.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Arusha, Halifax Masukiri, alisema mkoa huo umejiwekea mikakati mbalimbali ya kuhakikisha inaongoza kwenye mitihani yote ya kitaifa.

"Hapa walimu na viongozi tumeweka mikakati yetu ambayo tunaamini tutaongoza kwa kila mtihani wa taifa utakaofanyika kuanzia darasa la nne hadi kidato cha sita," alisema.

Awali, Mkuu wa Shule ya Sekondari Ilboru, Denis Otieno, alisema shule hiyo ina wanafunzi 840 na walimu 69 huku akidai kuwa hadi sasa shule hiyo haina hatimiliki.

"Eneo la shule halijapimwa hivyo tunaomba serikali kulipima ili shule iwe na hatimiliki itakayosaidia kujua mipaka ya eneo la shule, lakini hati kutumika kusajili laini ya simu ya shule maana hadi sasa tumeshindwa kuwa na simu ya shule kutokana na kukosa hatimiliki," alisema.

Pia alisema ukarabati uliofanywa na serikali katika shule hiyo umechangia kuongeza ufaulu huku akisema shule imeweka mikakati ya kuhakikisha walimu wanakamilisha mada za masomo yote kila inapofika mwezi Mei ili kufanya vizuri zaidi kwenye mitihani.

# Wanaong'oa mawe upimaji ardhi waonywa

**Na Munir Shemweta**

SERIKALI imewaonya wamiliki wote wa ardhi wanaoharibu, kung'oa na kuhamisha alama za upimaji ardhi (beacons) na kubainisha kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria.

Taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini iliyotolewa jana, ilieleza kuwa ni kosa kisheria kufanya shughuli yoyote inayoweza kusababisha kuharibu, kung'oa au kuhamisha alama za upimaji.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa wizara imebaini uwapo baadhi ya wananchi wanaoharibu, kung'oa na kuhamisha alama za upimaji na kusisitiza kuwa kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

"Kutokana na kukithiri vitendo hivyo inawakumbusha wananchi wote kuwa mtu yeyote atakayebainika kuharibu, kung'oa, kuhamisha au kufanya shughuli inayoweza kuharibu alama za upimaji ardhi, atakuwa ametenda kosa la jinai na atawajibika kulipa faini Sh. 750,000 au kifungo cha mwaka mmoja jela au adhabu zote kwa pamoja," ilisema taarifa hiyo.

"Wizara imewaasa wananchi wote kutojihusisha na vitendo hivyo kwa kuwa vinarudisha nyuma jitihada za serikali za kuongeza usalama wa miliki ardhi kwa wananchi," iliongeza.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa ikipanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa lengo la kuongeza usalama wa miliki za ardhi kwa wananchi na maeneo yote yaliyopangwa na kupimwa yamewekewa alama za upimaji ardhini kwa mujibu wa Sheria ya Upimaji Ardhi Sura ya 324.



Mkazi wa Goba, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, akifua nguo kwenye Mto Tegeta, kutokana na eneo hilo kukosa maji salama ya bomba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC awawashia moto wazazi wanaowaozesha wanafunzi

**Na Anthony Gervas,** MAGU

MKUU wa Wilaya ya Magu, Salum kalli, ameonya kuwa wazazi watakaobainika kuozesha watoto wao na kuwakatisha masomo, watakamatwa na kuwekwa gerezani siku 20 kabla ya kufikishwa mahakamani.

Kalli alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu watoto wa kike wanaokatisha masomo yao kutokana na kuozeshwa na wazazi wakiwa na umri mdogo.

"Wazazi wa pande zote watakaobainika wakiwaozesha watoto wa shule na kuwakatisha masomo na wale wanaowapa ujauzito wote kwa pamoja watakuwa ni kundi moja, tutawakamata na kuwaweka gerezani kabla ya kesi kuanza," alisema Kalli.

Alisema wanaohusika kuwapa mimba na kuwaozesha wanafunzi ndoa za utotoni watashughulikiwa na serikali ipasavyo kwa kuchukuliwa hatua kali.

Kalli alisema wapo watoto wanaozeshwa na wazazi wakiwa na umri chini ya miaka 15 kwa tamaa ya kupewa ng'ombe na kusababisha kukatisha ndoto zao za baadaye wakati serikali imejenga shule za msingi na sekondari kwa ajili ya wao kupata elimu.

Mkuu huyo aliwataka wazazi kuhakikisha watoto wao hawarubuniwi kwa kuwasimamia na kuwaelekeza maadili mema ili kuepuka mimba na ndoa za utotoni.

Kalli alisema yako makundi ya vijana yanayowafanyia ukatili watoto wa kike kwa kuwapiga na kuwabaka na kusema kuwa serikali itawashughulikia kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Pia aliomba mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha katika kupinga ukatili wa kijinsia kusaidiana na serikali kuwabaini wanaohusika na vitendo hivyo ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao.

# NHIF yawasajili wanachama 2,300

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Ruvuma umesajili wanachama 2,298 kutoka kundi la wanafunzi na wanachama wa vyama vya ushirika (AMCOS) kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Meneja wa Mfuko huo Mkoa wa Ruvuma, Hance Mwankenja, huku akibainisha kuwa makundi mengine yaliyojiunga ni ya watu binafsi, watoto, wafanyakazi toka taasisi za watu binafsi na mashirika ya dini.

Alisema jitihada kubwa zinafanyika katika kuhakikisha mwananchi mmoja mmoja anafikiwa ili kujiunga na mfuko kupitia mpango wa vifurushi na TOTO Afya kwa watoto walio chini ya miaka 18.

Kwa mujibu wa Mwankenja, kundi la vijana wa bodaboda, madereva, mama lishe na machinga limewekewa mpango kabambe kwa ajili ya kuwahamasisha na kujiunga na mfuko huo.

Hata hivyo, Mwankenja alisema katika kutekeleza shughuli za mfuko huo, nguvu kubwa itaelekezwa kwa wakulima walio kwenye AMCOS na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Aliongeza kuwa malengo ya mkoa ni kuendelea kuwafikia wanachama wapya kwa kutoa elimu ya bima ya afya ili kila mwanachama ajue na kutambua umuhimu wa kuwa na kadi ya bima hiyo kabla hajapatwa na majanga ya kuugua.

Pia alisema mfuko huo umesajili zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na za mkoa pamoja na maduka ya dawa wilayani kote kwa ajili ya kuimarisha huduma bora kwa wanachama.

Mwankenja alisema NHIF Ruvuma inatarajia kuongeza idadi ya wanachama kupitia makundi mbalimbali yakiwamo ya ushirika afya, wanafunzi, vikundi vya wajasiriamali pamoja na Toto Afya kadi.

# Wilaya yapewa mabilioni ya maji

Na Said Hamdani, LINDI

SERIKALI imejipanga kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya maji inakamilika kwa lengo la kuiondolea Jamii changamoto ya upatikanaji huduma hiyo, kwa kuipatia Wilaya ya Lindi, mkoani hapa jumla ya Sh. bilioni 8.0 kwa ajili ya utekelezaji wake kipindi cha mwaka 2020/2021.

Mkuu wa wilaya hiyo, Shaibu Ndemanga aliyaeleza hayo, alipokuwa anahutubia wananchi wa Halmashauri ya Mtama, katika mkutano wa hadhara kuazimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Akizungumza na wananchi hao, Ndemanga alisema fedha hizo zimeanza kufanyakazi kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kuanzia Kijiji cha Namunda, Kata za Ruhokwe, Mtua, Shuka, Rutamba na maeneo mengine ya wilaya hiyo.


Ndemanga alisema lengo la Serikali ni kuhakikisha wanawake ambao ni wawajibikaji wakubwa kwa masuala ya maendeleo wanaondokana na kikwazo katika upatikanaji wa huduma za maji mbali na maeneo wanayoishi.

"Serikali imeamua kuzitoa fedha za miradi hii, lengo lake kuu kumtua mama ndoo kichwani, na zimeanza utekelezaji wake," alisema Ndemanga.

Alisema Serikali imeendelea kujipanga kutatua changamoto hiyo, kwa kukamilisha mradi mkubwa wa maji kutoka Tarafa ya Nyangamara hadi Nyangao, kwa kujenga benki kubwa lenye ujazo wa zaidi ya lita milioni moja, yatakayosambazwa maeneo yote ya Mtama na Kata ya Nyangao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Yolenda Makumbuli, alitaja vikwazo wanavyokumbana navyo ni jamii kutokuwa tayari kushirikiana na vyombo vya sheria, Polisi na Mahakama pale wanapofanyiwa vitendo vya kikatili.

Vingine ni baadhi ya wanaume kutelekeza familia zao na kuwafanya wanawake kuwa na mzigo mkubwa wa kulea watoto peke yao.



Wanafunzi wa kidato cha kwanza wa shule mpya ya Sekondari Kigera, Kata ya Nyakatende, wilayani Musoma, mkoani Mara, ambayo ilifunguliwa rasmi Februari mwaka huu, wakiendelea na masomo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Watoto wa kike kupewa maelfu ya taulo

Na Mwandishi Wetu

KATIKA kuthamini mchango wa wanawake kwa maendeleo ya taifa, Kampuni ya Total Tanzania imejitolea kuunga mkono juhudi zote za kuwajengea uwezo watoto wa kike.Imekuja na kaulimbiu ya 'ukijaza mafuta kituo chochote cha Total Tanzania, unakuwa umesaidia kuchangia maendeleo ya wanawake wa Tanzania'.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa kampuni hiyo, Marsha Msuya Kilewo, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa Kampuni ya Total, yaliyofanyika katika kituo chake cha mafuta cha Oysterbay jijini Dar es Salaam kwa udhamini wa kununulia taulo za kike, zaidi ya wanafunzi 1,500 kutoka familia maskini, wasio na uwezo wa kununua taulo hizi. Udhamini huo unafanyika kwa ushirikiano wa ubia na Taasisi ya Flaviana Matata Foundation.

Marsha amesema kila mwezi, watoto wa kike hukosa shule siku 5 hadi 7 wanapokuwa kwenye siku zao kutokana na kukosa taulo za kike, hivyo kukosa masomo kwa siku 60 hadi 84 kwa mwaka kwa kushindwa kununua taulo za kike.

"Hivyo Total Tanzania pamoja na Flaviana Matata Foundation tunashirikiana katika kuhakikisha kuwa watoto wa kike hawakosi shule kwa kuwapatia wanafunzi ambao wametoka kwenye familia duni taulo za kike zaidi ya 9,000.

Hii ni kwa ajili ya kumpatia mtoto wa kike ujasiri wa kujiamini hata wakati akiwa kwenye siku zake na kuwa na uwezo sawa na mtoto wa kiume katika kutafuta elimu. Hivyo mwezi huu kwa kila Sh. moja ya kila lita ya mafuta itakayouzwa kwenye vituo vyetu vya Total itachangia kununua taulo za kike kwa ajili ya wanafunzi", alisema Marsha.

Kwa upande wake, Flaviana Matata, aliishukuru Total kwa kuwajali Watanzania, na kusema: "Ukimsaidia mtoto wa kike, ni umeisaidia jamii, msaada huo wa Total Tanzania, utasaidia sana kuwajengea uwezo watoto wa kike, hivyo kuwajengea uwezo Watanzania."

## Shule ya wenye ulemavu yapungukiwa madawati

Na. Deogratius Nsokolo, KIGOMA

SHULE Maalum ya Msingi Uvinza yenye wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali na mahitaji maalum wilayani Uvinza mkoani Kigoma, inakabiliwa na upungufu wa madawati, walimu na miundombinu, hali inayosababisha baadhi ya wanafunzi kusomea chini na kulala zaidi ya mmoja kitandani.

Mwalim Mkuu wa shule hiyo, Goma Kamani, alimwambia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyetembelea shule hiyo kuwa shule hiyo ambayo ni jumuishi ina wanafunzi 480 kati yao wenye ulemavu wa aina mbalimbali ni 197 ambao wana ulemavu wa macho, ulemavu wa viungo, ulemavu wa akili, ulemavu wa macho, viziwi na bubu.

Alisema kwa sasa shule hiyo ina walimu sita wanaofundisha elimu maalum na wana uhitaji ya walimu 20, na kwamba kutokana na ukosefu wa madawati, wanafunzi wanasoma wakiwa wamekaa chini, hali ambayo inaathiri uwezo wao wa kujifunza.

Kamani alisema kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi, wengine wanalazimika kulala wawili wawili, huku mazingira ya mabweni yakiwa katika hali isiyoridhisha kutokana na uchakavu.

Alisema wameshindwa kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili, baada ya fedha kiasi cha Sh. milioni 150 walizopewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Sh.milioni 12 zilizotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Uvinza kwisha, huku kazi ikiwa haijakamilika.

Walimu wa shule hiyo wameiomba serikali kusaidia kuondoa kikwazo hicho ili watoto hao wasome kikamilifu.

Prof. Ndalichako alisema shule hiyo inatakiwa kupewa kipaumbele na kuhakikisha inapata mahitaji ya msingi ili watoto hao waweze kusoma.

"Mazingira hapa ni magumu sana kwa walimu na wanafunzi,ni vizuri kila kiongozi akaona na kuchukua hatua, sasa shule kama hii mkurugenzi alipaswa kuipa kipaumbele cha kwanza, lakini hajafanya, hawa ndio wanyonge ambao wanapaswa kusaidiwa," alisema.

## Dar wapewa fursa ya matibabu bure macho

Na Yasmine Protace

WAKAZI wa Mkoa wa Dar es Salaam, wametakiwa kujitokeza kupata huduma bure za upimaji wa presha ya macho na kupatiwa ushauri.

Huduma hiyo ni ya siku tatu mfululizo, ambayo itatolewa na wataalamu wa macho kutoka katika Hospitali ya CCBRT kwa kushirikiana na Sun Pharma.

Hayo yalisemwa na Dk. Cycpian Ntomoka, Mkuu wa Idara ya Macho CCBRT.

Huduma hiyo ilianza jana na itaendelea hadi kesho katika Hospitali ya CCBRT.

Alisema ugonjwa wa presha ya macho unatajwa na wataalamu wa afya ya macho duniani kuwa wa pili katika kusababisha upofu usioweza kutibika na hutokea pale ambapo mshipa wa fahamu unaopeleka mawasiliano kwenye ubongo unaposhambuliwa kutokana na presha kali.

Aliongeza kuwa ugonjwa wa presha ya macho unasababisha uoni wa jicho kutorejea, isipokuwa kupitia matibabu jicho linaweza kutengamaa na kuzuia ugonjwa kuendelea kuumiza mshipa wa fahamu.

## Azaki zaitwa vita dhidi ya TB

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

ASASI za kiraia kisiwani Pemba zimetakiwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) katika kuhakikisha wanatokomeza ugonjwa wa kifua kikuu, ambao unaathiri jamii siku hadi siku.

Akizungumza na wanachama kutoka asasi za kiraia pamoja na watu wa tiba asilia, katika Ukumbi wa Ofisi ya UKIMWI Machomane Chake Chake, Dk. Khamis Abubakar kutoka kitengo shirikishi Kifua kikuu, homa ya ini, UKIMWI na ukoma Zanzibar, alisema ushirikiano unahitajika katika kuhakikisha ugonjwa huo unamalizika.

Alisema kifua kikuu kipo, ingawa wenye dalili hawafiki kwenye vituo vya tiba, hivyo kupitia asasi za kiraia pamoja na watu wa tiba asilia, washirikiane na Serikali kuwatafuta wagonjwa hao, jambo ambalo litasaidia kuwagundua mapema na kuzuia kuambukiza wengine.

Mratibu wa kitengo shirikishi kifua kikuu, homa ya ini, UKIMWI na ukoma Kanda ya Pemba, Hamad Omar Hamad, alisema lengo la mkutano huo ni kuibua kesi za ugonjwa wa kifua kikuu ambazo zipo mitaani ili kuwatibu wagonjwa hao.

"Watu wa tiba asilia wanapowafuata kuwa mgonjwa ana dalili za TB mwelekezeni kituo cha afya kwa ajili ya uchunguzi, hii mtatusaidia sana kuyaondosha maradhi haya", alieleza mratibu huyo.

Alisema elimu inahitajika zaidi katika kuhakikisha inawafikia wanajamii walio wengi, ili kuepusha maambukizi kwa wengine, kwani mtu mmoja mwenye TB anaweza kuambukiza watu kumi hadi 20 kwa mwaka.

Aidha alisema, matumizi mabaya ya dawa za kifua kikuu yanaweza kusababisha kifua kikuu sugu, ambacho kinachukua muda mrefu kutibika, hivyo atakaegundulika anatakiwa awe na msimamizi mzuri, ambae atamfanya mgonjwa kutumia dawa kwa uangalifu.

Mkuu wa kitengo hicho Pemba, Hasnuu Fakih Hassan, alisema watu wa tiba asilia wana mchango mkubwa katika kupiga vita ugonjwa wa TB, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake apambane, ili ifikapo mwaka 2035 kiwe historia.




Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Ukombozi katika Kijiji cha Mfyome, Kata ya Kiwere, Tarafa ya Kalenga, mkoani Iringa, akinawa mikono shuleni hapo jana, kama sehemu ya kujikinga na magonjwa yanayotokana na changamoto ya upumuaji, ikiwamo Corona. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Wanavijiji wakoshwa ukombozi wa maji

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WAKAZI wa vijiji vya Halmashauri ya Wilaya Iringa mkoani iringa ambao walikuwa wanatembea umbali mrefu kufuata huduma ya majisafi na salama, wameipongeza Serikali kwa kufanikisha ujenzi wa miradi ya maji.

Wakizungumza wakati wa ziara ya kamati ya siasa ya CCM ya mkoa, wananchi hao walisema kwa miaka mingi wamekuwa wakisumbuliwa na kero ya maji kwani maji yalikuwa yanapatikana mbali, lakini pia usalama wake haukuwa wa kuaminika, jambo ambalo lilikuwa linawasababishia kadhia ya magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu. Barika, mkazi wa kijiji cha Izazi, aliishukuru serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) kuwa miradi ya maji imepunguza tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika kijiji chao.

Alisema awali walikuwa wanatembea umbali mrefu kutafika maji, hali iliyozua migogoro katika ndoa kwa vile kinamama walikuwa wanatumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo.

Tumaini Mpogola, alisema walikuwa wanapata maji kwenye korongo, jambo ambalo lilikuwa linahatarisha afya zao, na walikuwa wanapokezana na wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi na punda, lakini sasa maji yanatoka vituoni kwa saa 24.

Naye, Richard Luhala, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mfyome katika Kata ya Kiwere, aliishukuru serikali kwa kukamilisha ukarabati wa mradi wa katika kijiji chao.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RWSS)), Masoud Samila, alisema kuwa Kijiji cha Izazi asilimia 96 wakazi wamefikiwa na mtandao wa maji zimebaki tu asilimia 4.

## Kibano ujenzi holela chaanza

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Tabora imeanza msako kwa wanaojenga nyumba bila kuzingatia mambo yaliyo katika Mpango kabambe wa ujenzi wa mwaka 2015 hadi 2035 kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Tabora, Bosco Nduguru, wakati akijibu maswali ya madiwani kwenye kikao cha robo ya pili ya Baraza.

Alisema katika mpango huo nyumba za sasa zinazopaswa kujengwa katika kata za Kanyenye, Gongoni, na baadhi ya maeneo ya kata za Chemuchumu, Tambukareli na Mbugani zinapaswa kuwa za ghorofa na sio nyumba za kawaida.

Nduguru alisema watu wote watakaobainika kujenga nje ya utaratibu watasimamishwa na kulazimika kuzibomoa ili kuruhusu ujenzi wa maghorofa.

Aidha, aliwataka watu wote wanaomiliki nyumba katikati ya Manispaa ya Tabora kuacha tabia ya kuuza nyumba zao bali wanapaswa kuingia ubia na watu wanaotaka kujenga majengo ya ghorofa na wao kuwa na eneo katika jengo.

Alisema katika kuhakikisha wanadhibiti ujenzi wa nyumba ambazo hazipo katika mpango kabambe wao, amemwagiza Kaimu Mkaguzi wa Majengo, Mohamed Mussa, kupita kila siku katika maeneo mbalimbali kuangalia majengo yanayojengwa.

## 'SMZ inaleta mabadiliko wanawake kuwa viongozi'

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, amesema Serikali ya Zanzibar ya awamu ya nane inaleta mabadiliko ya kasi kwa wanawake kushika nafasi za uongozi kwenye ngazi za uamuzi.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani, na kuwa, kila mmoja anaona nchi inavyoleta mabadiliko ya kasi kwa viongozi wanawake kuingia kwenye ngazi za uamuzi, hivyo ipo haja kwa waandishi kuelimisha zaidi jamii na Serikali, ili kuhakikisha kwamba inamwinua mwanamke.

"Tuendelee kuelimisha kwa hali ya juu ili ifike pahala tutambue uoni na mtazamo wa jamii na Serikali juu ya kumwinua mwanamke, kwani sehemu anapokuwapo mwanamke na maendeleo yanapatikana kwa haraka", alisema Mkuu huyo.

Aidha alieleza kuwa, zamani wanawake hawakupata fursa ya kusoma, jambo ambalo limesababisha kukosekana viongozi wanawake katika vyombo vya kutoa uamuzi.

Ofisa Uwezeshaji wa Wanafunzi wa Kike na Vijana kupitia elimu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Viola Muhangi Kuhaisa, alisema elimu inahitajika zaidi katika kuhakikisha wanajamii wanapata njia bora ya kutatua vikwazo vinavyowakabili wanawake na watoto. "Tunapigania haki za wanawake na watoto, ili wasipatwe na udhalilishaji wa aina yeyote na kuhakikisha wanakuwa salama dhidi ya ukatili, ubakaji, ndoa na mimba za umri mdogo," alieleza.

# ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI MACHI 11, 2021



Ukurasa 12

TATIZO MIGUU KUPINDA...

**Mila potofu imeshikilia chanzo cha ulemavu wa watoto nchini**



Ukurasa 13

Mkurugenzi Kinga na darasa la mbu, nzi vita vya malaria, usubi, kichocho



Ukurasa 14

KITENDAWILI CHA MAHARAGWE

**'Mboga ya Taifa' katika mapito gharama mkaa na mbadala gesi**

# Darasa la shida kuu ya dawa 'feki' zilizoisha muda wake

Na Sabato Kasika

DAWA ni sehemu ya maisha ya mtu. Kiasi kidogo kinachotumika kutibu magonjwa, kinapatikana katika mazingira wanayoishi, pia zikiwa na kemikali baada ya kuzalishwa viwandani.

Wataalamu wa afya wanashauri watumiaji kuwa makini katika utupaji zilizoisha muda wake, ili kuepuka madhara ya kiafya na uharibifu wa mazingira.

Hivyo, haitakiwi kutupa dawa za binadamu, vipodozi, dawa za mifugo na nyinginezo katika jalala, inachangia ongezeko la kemikali katika mazingira.

Inaelezwa kuwa dawa zinazoandikwa na daktari na zile zinazoweza kununuliwa bila kuandikwa na daktari kutoka katika duka la dawa, zinapotupwa jalalani au kwingineko kuflashi chooni na kwenye sinki la kunawia, kemikali zake zanaweza kuingia katika maji safi na hata udongo.



Dawa aina mbalimbali. **PICHA: MKATABA**

## MFAMASIA DARASANI

Mfamasia Michael Mbasha wa Chuo na Famasia cha Nnobo, jijini Dar es Salaam, anasema madhara yake yanaweza kuwa ya viumbe ardhini, hata binadamu wa kada tofauti.

Mbasha anawaasa watumiaji wasitupe ovyo dawa zilizoisha muda wake, badala yake waangalie famasi zilizo tayari kukusanya dawa zilizoharibika na kuziharibu katika njia iliyo sahihi.

"Famasi za hospitali za serikali zimekuwa na mpango huo kwa dawa mbalimbali zitumikazo hospitalini hukusanywa na kuharibiwa kwa njia sahihi badala ya kutupa jalalani au kwingine kusikotakiwa," anasema Mbasha.

Mtaalamu huyo wa dawa, anasema ukusanyaji dawa zilizoharibika au kwisha muda wake, ni njia sahihi ya kuziharibu, jambo litakalowalinda.

"Usitupe chooni au kuchimbia ardhini dawa zilizoisha muda wa matumizi, kwani zinapaswa kuteketezwa kwa utaratibu maalumu na kama mtu hajapewa maelekezo ni kuziteketeza ni bora azirejeshe kwa mfamasia," anasema.

Mbasha anasema, dawa zilizokwisha muda wake, zitakapochimbiwa ardhini au kutupwa chooni, ni hatari, sumu kwa mazingira na viumbe mbalimbali wanaoishi karibu au umbali mdogo.

Mtaalamu huyo anasisitiza: "Kama famasi zilizo karibu hazina mpango wa kuteketeza dawa hizo, ni vyema kuwasiliana na watu wa mazingira, ili kujua kama waneweza kukusanya dawa zilizoisha muda wake na kuziharibika kwa njia sahihi.

"Pia, kama mtu hana uhakika kuwa dawa yake ni salama kwa matumizi, ni vyema aende akamuone mfamasia katika famasi iliyo karibu ili kupata maelekezo ya kitaalamu kwa ajili ya usalama wa afya yake."

Anasema, kuna haja kila mtu kuangalia angalau mara moja kwa mwaka kabati lake la dawa na kuondoa ambazo hazitumii akazipeleka mahali sahihi pa kuziteketeza.

Pia, katika matumizi binafasi anasema mtu anapaswa kutumia dawa alizoandikiwa na daktari au amepewa kutoka mamlaka sahihi kama famasia, ikizingatiwa na namna na wakati anaopaswa kutumia.

"Vilevile anatakiwa kujua achukue hatua gani unapokuwa umesahau kumeza dawa au anapopata madhara yasiyovumilika yatokanayo na kutumia dawa hizo," anasema.

## DAWA INAVYOTUMIWA

Anashauri, kila mtumiaji dawa kuwa makini kusoma muda wa kwisha matumizi ya dawa anayonunua, ili kuepuka madhara kiafya yanayoweza kumpata, atakaponunua zilizoisha muda.

"Ninajua kuwa wapo watu wengi tu ambao hununua dawa bila kuangalia muda wa matumizi, matokeo yake wanauziwa hata zile zilizopitwa na wakati, hali ambayo ni hatari kiafya," anasema.

Anafafanua kuwa dawa ambazo muda wa matumizi umeisha, huwa zinapungua nguvu, hata mtu akipewa dozi, hawezi kupona, badala yake zinaweka usugu na sumu kwenye mwili.

"Vilevile matumizi ya dawa zilizoisha muda wa matumizi zina athari kiuchumi, kwani mgonjwa anaweza kulazwa hospitalini kwa muda mrefu, hivyo kuwafanya ndugu zake kutumia gharama kubwa kumhudumia," anasema.

Anasema, mgonjwa anaweza kulazwa kwa muda mrefu, kwa vile hata dawa mpya anazopewa zinaweza kuchukua muda mrefu kufanya kazi kutokana na usugu wa zile za awali alizotumia bila kujua kuwa zimeisha muda wa matumizi.

"Sasa katika mazingira hayo, ni wazi kuwa kutakuwa na athari za kiuchumi, kwani hata mgonjwa mwenyewe badala ya kutibiwa na kuondoka kwenda shughuli za uzalishaji, inabidi akae muda mrefu hospitali.

"Ukifuatilia vyombo vya habari, utasikia baadhi ya watu wasio waaminifu wanakamatwa wakiuza dawa ambazo muda wa matumizi umekwisha, hivyo ni wazi wameumiza wengi, jamii iwe makini," anahitimisha.

AFYA

TATIZO MIGUU KUPINDA...

# Mila potofu imeshikilia chanzo cha ulemavu wa watoto nchini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TATIZO la ugonjwa wa 'mguu kifundo' nchini (clubfoot) kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, linatajwa kuchangia ongezeko la ulemavu kwa kundi hilo, kutokana wazazi na walezi kuwafungia ndani tangu kujifungua, wakihusisha na imani za kishirikina.

Wakati Tanzania ikiwa haina taarifa sahihi inayojulikana juu ya watoto wangapi wenye miguu kifundo na kwa kutumia viwango vya matukio ya kimataifa na idadi ya watu na viwango vya kuzaliwa nchini.

Taarifa za Asasi ya Kusimamia Wenye Matatizo ya 'Mguu Kifundo' (TCCO), inakadiria kila mwaka ni kati ya watoto 2,200 na 3,000 wanapozaliwa nchini wakiwa na miguu kifundo.

Pia inakadiria watoto 1,813,000 wanaozaliwa na miguu kifundo kila mwaka duniani, theluthi moja yao wanatoka nchi zinazoendelea au kukua kiuchumi.

Ingawaje chanzo chake hakiko bayana kitaalamu, lakini kuna ubashiri wa kitaalamu kwamba kisababishi kikuu ni maumbile na mazingira yanayowazunguka. Pia watoto wanazaliwa katika familia zenye historia ya tatizo hilo.

Hilo limekuwa likijitokeza baada ya mjamzito kujifungua na kuona miguu au mguu wa mtoto umepinda, wengi kati yao wanaoishi vijijini huwafungia kuhusisha hilo na imani za kishirikina zilizojengeka vichwani mwao.

Kunatajwa hali kuwapo kawaida watoto wa umri chini ya miaka mitano kupata ulemavu wa kudumu, sababu kuu ni kushindwa kuwafikisha kwenye matibabu, wakithamini mbadala wa waganga wa jadi.

Inaelezwa, TCC0, kwa kushirikiana na serikali, pia mdau muwezeshaji asasi ya Miracle Feet, walianzisha vituo vya utoaji huduma hiyo kitaifa, kuazimia kuwafikia wazaliwa wenye shida hiyo na hadi sasa ina jumla ya vituo 40 kitaifa, kutoka 25 za mwaka 2014.

Mathalan, hivi sasa katika Kanda ya Ziwa viko vituo 16 vinavyotoa matibabu bure kwa wenye tatizo hilo, bila ya kujali wanakotoka.

### WAGONJWA WAFUNGUKA

Kinigo Matelemba (37), anayeishi kijijini Nduku, katika Manispaa ya Kahama, pia NI muuguzi katika zahanati ya kijiji hicho, anasema aligundua tatizo wiki moja tangu mtoto azaliwe Machi mwaka jana, miguu ikiwa imepinda

Anasema, alichukua hatua haraka kumfikisha hospitali kwa matibabu, huku mkewe akiwa na hofu kubwa huenda mtoto umefanyika yshirikina, jambo ambalo halikuwa sahihi.

Matelemba anasema, alianza kumjenga mama huyo kisaikolojia na mpaka sasa ana mtoto wa miaka miwili anayeendelea na matibabu, miguu imenyooka.

Aidha, anasema mpaka sasa, kila baada ya wiki tatu anampeleka mtoto kliniki kuchunguzwa hadi atakapofikisha umri wa miaka mitano, ndio itakuwa mwisho wa hatia hiyo ya matibabu.

Simulizi hizo zinaendelezwa na Regina Maige (20), kutoka Kata ya Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu, anayesema kabla ya mwanawe kupatiwa matibabu ya miguu, mwanzo alihisi karogwa na alimfungia ndani kukwepa alichokihisi kuwa: "aibu kumzaa mtoto mlemavu."

Maige anaeleza ukombozi wa mwanawe ulianzia kujitokeza kwa mama kijijini, aliyekuwa na mtoto mwenye tatizo la aona hiyo na akamshauri waende kwenye kituo cha afya, akimsisitizia ugonjwa huo unatibika.

Ni hatua iliyowafikisha hadi Hospitali ya Manispaa ya Kahama, umbali wa zaidi ya kilomita 100 na sasa mtoto mwanawe anatembea, huku wakiendelea na matibabu.

Mwanamama Rehema Emmanuel, anadokeza masahibu yao wanatengwa kifamilia, kila baada ya kujifungua. Ni jambo linalohusishwa na ushirikina, hali ambayo mara nyingi inawasuritisha hasa wazazi wa kike wanaenda kutafuta majibu kwa waganga wa jadi, watoto wanaishia kwenye ulemavu wa kudumu.



Kinigo Matelemba kutoka kijijini Nduku, Kata ya Kinaga katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, akiwa na mwenzake wakisubiri kumwona daktari, kupata maendeleo ya afya ya miguu ya mtoto wao. **PICHA: SHABAN NJIA**

> **Ukombozi wa mwanawe ulianzia kujitokeza kwa mama kijijini, aliyekuwa na mtoto mwenye tatizo la aina hiyo na akamshauri waende kwenye kituo cha afya, akimsisitizia ugonjwa huo unatibika.**

### MADAKTARI WA MIFUPA

Dk. Homorina Mfoi, Mkuu wa Kitengo cha Mifupa na Viungo katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa Kahama Mjini, anasema ni muda mrefu hadi mwaka 2014, ndio walianza kutibu adha ya vifundo.

Anasema, hadi sasa wameshatoa huduma kwa watoto 285, kati yao wanane walipona na kuruhusiwa; waliokimbia hawajulikani waliko 10; na 50 wamekuwa wakikumbushwa ratiba za matibabu kila inapowadia siku za kliniki.

Dk. Mfoi anasema, mwitiko umeongozeka maradufu akijivunia wigo unaopanuka, Hospitali ya Kahama inapokea wagonjwa kutoka wilaya za mikoa jirani kama Kaliua, Nzega, Mbogwe, Geita, Kakonko na Kibondo.

Anasema, ni mwitiko unaotokana na elimu wenayotoa kwa kinamama wajawazito wanaofika kliniki, wakipatiwa vipeperushi wanavyokwenda kuwapatia wenyeviti wa vijiji na watendaji kata.

"Ugonjwa wa mguu kifundo hauko Tanzania tu, upo dunia nzima na nchi inayoongoza kwa ugonjwa huo ni nchi ya India. Ugonjwa huu unatibika hasa pale mzazi anapofuata maelekezo atakayopewa na daktari na sio kuamini ugonjwa huo unatokana na kurogwa," anasema Dk,Mfoi.

### WAGANGA WA JADI NAO

Dk. Mfoi anasema wanatarajia kufanya vikao na waganga wa jadi, ili kuwapatia elimu ya tatizo la mguu kifundo, ili nao wachangie kuwashauri wateja wao kufika hospitalini wakatibiwe.

Mtaalamu wa viungo, Dk. Boniphace Mwero, anasema ,matibabu yako ya aina mbili, marekebisho ya mguu au miguu na kushikilia marekebisho na baadae mtoto kufungwa 'muhogo' kila wiki, hatua inayochukua wiki tano hadi nane.

Daktari anataja hatua inayofuata ni kufanyika upasuaji mdogo unaorefusha kamba za miguuni kwa wiki tatu, mtoto anavalishwa 'gango pinde' (kiatu maalumu) kwa saa 23 kila siku ndani ya miezi mitatu.

"Ataendelea kuvaa viatu hivi saa 23 kila anapolala iwe mchana au usiku mfululizo kwa kipindi cha miezi mitatu. Baada ya miezi hiyo, ataendelea kuvaa na kuhdhuria kliniki kwa kipindi cha miaka mitano atakapokuwa anapona kabisa," anasema Mwero.

### HATUA NGUMU

Dk. Mfoi, anasema magumu wanayokutana nayo wakati wa utoaji huduma, ni wazazi kukatisha tiba za watoto, pindi wanapowaona wanaanza kutembea, pasipo kujua kwamba ni tatizo linaloweza kumrejesha mtoto katika hali ya awali.

Rai ya mtaalamu wa afya huyo, ni kwamba elimu inahitajika kwa wananchi watambue zaidi matibabu ya mtoto mwenye shida hiyo ya mguu, kila ifikapo miaka mitano tangu kuanza matibabu, inajengeka imani mtoto amepona na vigumu kurudia hali ya zamani.

Hata hivyo, anadai tatizo la baadhi ya wazazi kukimbia matibabu na unapofika msimu wa kilimo, wazazi wengi wanatumia muda zaidi shambani, badala ya safari za kumpeleka mtoto kliniki, hata kuchangia baadhi ya watoto waliokuwa katika hatua za mwisho kurudia shida ya zamani.

Dk. Mwero anasema, kwa watokao mikoa na wilaya jirani wamekuwa wakikatiza matibabu njiani kwa kukosa nauli ya kumfikisha kliniki kujua hali ya mtoto wake inaendeleaje, hivyo wamekuwa wamekuwa wakiwapigia simu kuwakumbusha na kusisitiza kufika kliniki.

Anasema kuwapo tabia ya baadhi ya wanaume kuwasitisha wenza wao wasiendelee kuwapeleka watoto kliniki, baada ya kuwaona wana hali nzuri wanatembea, jambo ambalo huwa inawarudisha tena kwenye ulemavu.

AFYA

# Mkurugenzi Kinga na darasa la mbu, nzi vita vya malaria, usubi, kichocho

**Na Yasmine Protace**

• Kinachojiri kwenye maradhi kwa hatua



Tabibu wa malaria akiwajibika na mgonjwa. **PICHA: MTANADAO**

MALARIA ni ugonjwa unaodhuru kwa wakazi wa ukanda wa tropiki, hasa pale mtu anapochelewa matibabu anayakaribisha majanga.

Kwa wajawazito, inatajwa kitaalamu ni hatari zaidi na kuwasababishia majanga kama vile upungufu wa damu na hatari ya kupoteza mtoto tumboni.

Mwenezaji mkubwa wa malaria ni mdudu mbu, mazingira yake yakihamsishwa na uchafu wa mazingira unaounda mazalia ya mbu.

Pia kuna magonjwa mengine kama matende yanaenezwa na mbu huyo, huku sura nyingine ya mdudu arukae, nzi naye yumo katika orodha ya kudhuru kwa kina kupitia njia hiyo.

**DARASA LA MALARIA**

Dk. Leonard Subi, Mkurugenzi wa Idara ya Kinga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto anatoa darasa akitamja mbu aina ya anopheles, ndiye mwenezaji mkuu wa malaria.

Anasema, hilo linafanyika kupitia vimelea vya plasmodia, kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Dalili za malaria ni mgonjwa kupata homa kali, anaharisha, kutapika, kuumwa kichwa, kutetemeka na maumivu mwili mzima.

Kwa watoto, inatajwa hatari inaweza kuwa mbaya na haraka sana, hasa kwa walio na umri chini ya miaka mitano, kwa sababu miili yao haijajenga kinga ya kutosha kukabiliana na malaria.

Dk. Subi anasema maisha ya wengine wengi yanaweza kuokolewa, kwa kuzuia na kuitibu mapema, hivyo wana haki ya kupata huduma nzuri za afya kwa ajili ya tiba bora ya malaria.

Katika kuhakikisha serikali inapambana na hatari ya malaria, Dk. Subi anasema jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanywa kupambana na ugonjwa huo.

Anasema, hadi sasa Tanzania imeshapiga hatua katika kuupunguza ugonjwa wa malaria, licha ya baadhi ya mikoa kuwa na maambukizi ya juu ya ugonjwa.

Dk. Subi, anatoa ufafanuzi huo wa kina katika ufunguzi wa kikao kazi cha kwanza cha wataalamu wabobezi wa kudhibiti wadudu waharibifu waenezao magonjwa, tangu kuanzishwa kwa kitengo chao nchini.

Anasema, hivi sasa kikosi hicho cha wataalamu kinaandaa mwongozo wa kukabiliana na wadudu waharibifu waenezao magonjwa, akiwamo mbu. Lengo ni kuishauri wizara mama njia bora za kukabiliana na wadudu hao.

> **Hadi sasa Tanzania imeshapiga hatua katika kuupunguza ugonjwa wa malaria, licha ya baadhi ya mikoa kuwa na maambukizi ya juu ya ugonjwa.**

Mkurugenzi wa Kinga anazitaja njia hizo, ni pamoja na udhibiti wa mazingira kwa kuhakikisha mbu na wadudu wengine waharibifu hawapati sehemu ya kuzaliana na kusambaza magonjwa.

Hoja ya usafi wa mazingira, ikiwamo uboreshaji nyumba kuzuia wadudu waharibifu, inajumuisha watu kulala kwenye vyandarua vyenye dawa.

Dk. Subi anatoa mfano katika kudhibiti mbu, vipo viuatilifu na viuadudu kuanzia na viluilui kwenye mazalia ya mbu, ambavyo anasisitiza haja ya kutumika bidhaa za viwanda vya ndani.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kuna umuhimu wa bidhaa za nchini, kwani taasisi za ndani ndizo zilizofanya utafiti na kuonyesha mafanikio makubwa ya mbu kupungua, pamoja mnyororo wa maambukizi.

"Matumizi sahihi ya vyandarua ni muhimu sana katika kudhibiti malaria, tunataka angalau zaidi asilimia 80 ya Watanzania walalie vyandarua vilivyoweka viuatilifu vya muda mrefu kumpunguzia mbu umri wa kuishi.

"Hivyo, kupunguza uwezekano wa kusambaza vimelea vya malaria ikiwa ni pamoja na upuliziaji wa viuatilifu ukoko ndani ya nyumba," anasema.

**NAMNA INAVYOENEA**

Mgonjwa huambukizwa kwa kuumwa na mbu jike mwenye vimelea vya plasmodium na kisha vinasambaa kwenye mfumo wa damu wa aliyeumwa.

Kuna vimelea zaidi ya 400 wanaoweza kuambukiza aina nyingi za wanyama kama wanyama, jamii ya mijusi na ndege.

Aina nne ndizo maarufu siku nyingi kueneza malaria kwa binadamu na katika hizo, ipo moja maarufu kuwaenezea nyani, ambayo kwa siku za karibuni imegunduliwa kuwa chanzo pia cha malaria kwa binadamu.

Jamii aina ya P.falciparum; anapatikana dunia nzima kwenye maeneo ya joto kali na la wastani, hasa Afrika.

Huwa anaweza kuleta malaria kali, kwa sababu anazaliana kwa kasi sana ndani ya damu na kusababisha upungufu mkubwa wa damu.

Pia ni vimelea wanaoweza kuziba mishipa midogo ya damu, hali ambayo ikitokea kwenye ubongo, anapatwa na 'malaria ya ubongo' huku hatari ya kifo inakuwa jirani.

P. vivax; anapatikana zaidi Bara Asia anakofahamika zaidi, Marekani ya Kusini na baadhi ya maeneo Afrika. Huwa ana vipindi vya kutulia kwa muda ana anapoamka anaweza kuamka kushambulia damu miezi au miaka kadhaa baada ya kuumwa na mbu.

P. ovale; anapatikana zaidi Afrika (hasa Afrika Magharibi). Anafanana kimaumbile na kibaiolojia na P.vivax. Tofauti yao, huyo ana uwezo mkubwa kushambulia baadhi ya watu.

P. malariae; anapatikana dunia nzima. Ni kimelea pekee cha malaria mwenye mzunguko wa siku tatu. Jamii zote tangulizi zina mzunguko wa siku mbili.

Hatari yake husababisha maambukizi sugu na hata kudumu maisha yote ya mgonjwa na athari mojawapo, ni kuharibu mishipa midogo ya damu ndani ya figo.

P. knowlesi; anapatikana maeneo Kusini Mashariki, mwa Asia kama kimelea anayeshambulia aina fulani za nyani. Amebainishwa kuambukiza aina ya malaria maarufu kwa nyani, hasa nchini Malaysia.

**KICHOCHO JE?**

Kwa upande wa ugonjwa kichocho, Dk. Subi, anasema kikosi hicho kitaangalia namna ya kudhibiti ugonjwa huo kwenye maeneo yenye majaruba mengi yanayoeneza maradhi hayo, ikiwamo katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

"Mbu wanaeneza pia matende na mabusha, dengue, (homa ya) chikungunya, homa ya manjano na magonjwa mengine yanayokuja kwa vipindi vya mvua, kwa hiyo tutapambana kwa kumwangalia mwananchi kudhibiti magonjwa hayo," anasema.

Dk. Subi kupitia nafasi yake, Mkurugenzi wa Kinga, anaongeza kuwapo inzi weusi (Simulium) wanaoeneza ugonjwa wa usubi, hususan kwenye mikoa ya Morogoro wilayani Mahenge, hali kadhalika Tukuyu, mkoani Mbeya.

Anasema hivi sasa kikosi hicho cha tiba kinaendelea na kazi yake mkoani Iringa, hivyo hivi sasa kinaangalia nafasi ya kuwadhibiti nzi hao wenye maambukizi, kuliko kuendelea kuwamezesha wananchi dawa kila mwaka.

Dk. Subi anawasisitiza wataalamu hao kuangalia namna wanavyoweza kutumia dawa za asili kufukuza na kuwaua mbu na wadudu wengine waenezao magonjwa, kupitia mbinu za kisasa.

***Imechangiwa na taarifa za mtandao.***

MAZINGIRA

KITENDAWILI CHA MAHARAGWE

# ‘Mboga ya Taifa’ katika mapito gharama mkaa na mbadala gesi

• Mlo mkuu kwa familia nyingi & mama lishe

**Na Nimi Mweta**

UKITAJA neno au jina, maharagwe, tayari inakuja picha pana kichwani inayoweza kutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Hata hivyo, vielelezo vyake havitatofautiana kwa kina.

Kwanza kuna hisia ya kuwa chakula cha kawaida kinachopatikana kwa ‘mama ntilie’ambao kuna wanaojitahidi kuita ngazi ya ‘mama lishe.’ Kubwa linaloiweka mahali hapo ni ile gharama husika ya kawaida.

Ni mlo uliozoeleka sehemu nyingi kutokana na sababu lukuki, kama mazoea ya kihistoria, bei na lishe inayopatikana ndani yake.

.Maharagwe ni chakula muhimu chenye protini ambacho hasa zaidi inapatikana kwa watu wa tabaka la chini, ambalo kwa lugha ya elimu jamii karne iliyopita lilikuwa linaitwa la ‘wafanyakazi.’ wanashindia mboga hiyo kwani ni rahisi na toshelevu kwa mahitaji ya kila siku.

Katika utani wa kawaida wa sasa, imebatizwa jina kuwa ‘mboga ya taifa’ kwa maana inapatikana takriban katika kila nyumba, hasa kwa umma unaoishi maisha ya kawaida.



Biashara ya mamalishe ikiendelea, ambako maharagwe ni sehemu ya bidhaa kuu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MTIHANI GHARAMA?

Ila kwa kawaida hata kwa mlo wa biashara za mama lishe, huchanganywa na mboga nyinginezo, hata iwe ni kwa mbali. Hivyo, endapo mboga ikikosekana, inabidi mpangilio wa chakula ubadilike, nyama au samaki waongezwe. Bila shaka gharama ya leo inapanda.

Siyo rahisi mtu akasema kiasi cha mboga kimekuwa mlinzi wa sera za vipato na hasa kuridhika kwa maisha kwa tabaka la chini, yaani wafanyakazi, kibarua, mkulima na wajasariamali na hata wahangaika mitaani wanaojulikana ‘deiwaka.’ Zamani kulikuwapo neno lililoendana na mazingira ya kazi wakati huo wakiitwa ‘kibarua,’ ishara ya stakabadhi wezeshi kufanya kazi kwa kipindi fulani, kama ni siku au wiki.

Inawezekana neno hilo halikusahaulika ila linaleta picha tofauti, mtu anajisikia aina fulani ya mtumwa, tofauti na ‘deiwaka.’

Bila ya maharagwe kuwapo, ingebidi wafanyakazi wa jumla walipwe kiasi kizuri cha fedha, ili wamudu gharama za mlo kama nyama ya ng’ombe au samaki za kutosha kuwawezesha kufanya kazi.

> **Imekuwa mlo wa wanaojimudu kiuchumi wanatafsiri, kama ambavyo wanaojimudu hutumia nyama zaidi au pekee na chakula cha nafaka kama ugali au wali.**



Maharagwe yaliyo tayari kwa kuliwa.

Imekuwa mlo wa wanaojimudu kiuchumi wanatafsiri, kama ambavyo wanaojimudu hutumia nyama zaidi au pekee na chakula cha nafaka kama ugali au wali.

Kwa mfano, mtu anapoagizwa mlo wenye kitoweo kama kuku; hakuna maharagwe anayoambatanishwa au ‘ugali rosti’ yaani nyama ya kukaanga, kimsingi inajitegemea. Mara zote bei za vyakula hivyo ni tofauti na ugali au wali wenye nyama na maharagwe.

Uhalisia uliopo ni bayana, katika nyumba nyingi mfano jiji la Dar es Salaam, zinahama kwa kasi kutumia gesi ya mitungi, badala ya mkaa ambao gharama yake kupikia vyakula vyote ndani ya nyumba ni zaidi ya mara mbili ya kutumia gesi.

Ila kuna tofauti kwa maharagwe, yakiwa rekodi ya usumbufu kuiva na kumaliza mkaa na gesi.

Wanaopika vyakula barabarani hasa mama lishe, hawana mbadala, zaidi ya kupandisha bei ya chakula anachoweza kula mtu akashiba kiasi cha kuridhisha.

### MWELEKEO SIKU ZIJAZO

Kutokana na ushindani miongoni mwao mama lishe, kupandisha bei za vyakula ni nadra na kutokana na gharama kubwa ya nishati hiyo, faida wanazopata zinapungua zaidi na kuwashusha kibiashara, baadhi kutoka kipato endelevu, hadi ‘ubangaizaji’ asiwe wa kukaa ndani tu.

Soko la mkaa, bidhaa inayokabiliwa na udhibiti kimazingira litaendelea kutesa kwa maana ya maeneo ya kukata miti kupungua na bei yake kutoshikika kwa ‘wabangaizaji.’

Ni uhalisi ambao hautakuwa rahisi iwe kina mama lishe au migahawa, haitakuwa rahisi kuendelea kutoa chakula chenye maharagwe kirahisi, kwani ndiyo chembe ya matumizi yao kwa jumla inayogharimu zaidi.

Ina maana itabidi wahamie katika maharagwe laini (yanaitwa ya Mbeya) au vyakula vinavyofanana nayo, ikiwa gharama yake kwa kutumia mkaa itakuwa rahisi zaidi, labda kama bidhaa hizo zinafanana, kwa mfano choroko.

Hatua inayofuata katika nishati ya kupikia kila mahali ni matumizi ya gesi na ili maharagwe yabaki katika mchanganuo wa kutayarisha chakula cha kawaida, itabidi zipatikane aina zenye tija kwa ‘mama ntilie’na migahawa ya kawaida.

Bado hakuna uhakika kama tatizo hilo limewahi kufanyiwa kazi, kwani inahitaji nchi yenye utamaduni wa chakula unaofanana, mfano nchi mojawapo jirani ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Njia mojawapo muhimu inayopaswa kuchukua nafasi ni pale asasi za utayarishaji chakula kibiashara zinapaswa kutafuta njia za kujaza nafasi ya maharagwe, endapo mkaa utazidi kupanda bei, Kwa ujumla, hakuna gharama rahisi.

Ipo njia ambayo kinamama wanafanya, kuyaloweka maharagwe usiku kucha ili yawe laini, na ingekuwa ni soya, kutoa maganda yake ili yaive kwa urahisi na hata kupoteza sumu ambayo wataalamu wanasema yana madhara kama yasipopunguzwa au kuondolewa.

Uloweshaji wa aina hiyo, mi aina mojawapo inayoweza kuwa mwarobaini wa hilo, hata hivyo, unazaliwa mtihani mwingine, mfano wateja wanapotaka vyakula kupikwa kwa mkaa badala ya gesi. Hapo kuna nyama, kwenye gesi inaivishwa kwa kuburuzwa haraka mno.

Inawezekana siku zijazo, kutokana na watu kuchangamkia hatua tofauti za uwekezaji, uzalishaji miti na uuzaji wake ukawa umeenea zaidi, lakini siyo rahisi kwa bidhaa kama hiyo kupunguza makali ya kutumika kupika chakula cha bei ya chini kabisa.

Ila bado kuna biashara ya nyama pori imeanza kuzungumziwa, ambayo si ajabu ikafumua kabisa soko la vyakula.



# Huduma matibabu MOI, Ocean Road zaokoa mabilioni ya fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHILINGI Bilioni 48.8 zimeokolewa na serikali kwa kutopeleka nje ya nchi wagonjwa wa saratani na mifupa kwa kipindi cha miaka mitano.

Hatua hiyo imetokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika huduma za kibingwa kwenye Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).

Akiwasilisha taarifa ya ORCI kwa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Julius Mwaiselage, alisema uwekezaji huo umepunguza rufani za wagonjwa wa saratani kwenda nje ya nchi na kuokoa Sh. bilioni 10.4 kwa kutopeleka wagonjwa 208 nje ya nchi.

Alisema uwekezaji huo umefanywa kwenye kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za kibingwa katika taasisi hiyo uliohusisha ununuzi wa mashine za kitaalam na ujenzi wa majengo.

"Uwekezaji huu umepunguza rufaa (rufani) za wagonjwa wa saratani kwenda nje ya nchi kutoka wagonjwa 164 mwaka 2014/15 hadi wagonjwa watano mwaka 2019/20," alisema.

Pia alisema wagonjwa wanaotoka nchi jirani kwa ajili ya tiba wameongezeka kutoka wagonjwa 12 mwaka 2014/15 hadi 73 mwaka 2019/20, hivyo kuongeza mapato kwa serikali.

"Miundombinu tuliyonayo sasa idadi ya wagonjwa wanaotibiwa kwa siku imeongezeka kutoka wagonjwa 170 hadi wagonjwa 270," alisema.

Mwaiselage pia alisema taasisi hiyo imepunguza muda wa kusubiri tiba mionzi kutoka wiki sita mwaka 2014/15 hadi wiki mbili mwaka 2019/20 muda ambao ndio kiwango kinachokubalika cha kusubiri tiba duniani.

Kwa upande wa MOI, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Vivina Wananji, alisema kwa kipindi hicho taasisi hiyo imefanya upasuaji wa kibingwa kwa wagonjwa 43,200.

Alisema kwa gharama za hapa nchini, upasuaji huo umegharimu Sh. bilioni 16.5 na kama wangepelekwa nje ya nchi matibabu yangegharimu Sh. bilioni 54.9, kwa mantiki hiyo, alisema Serikali imeokoa Sh. bilioni 38.4.

Dk. Wananji pia alisema serikali imetoa Sh. bilioni 7.9 kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya kisasa ya upasuaji wa ubongo.

"Maabara hii itaiwezesha taasisi kufanya upasuaji wa matatizo ya mishipa ya damu kichwani pasipo kulazimika kufungua fuvu la kichwa, vilevile mashine hii itakua na uwezo wa kutibu damu iliyoganda kwenye mishipa ya damu miguuni, kwenye moyo, tumbo la uzazi, ini na figo,"alisema

Alisema matibabu kwa kutumia maabara hiyo ni ya haraka hivyo wagonjwa wengi watapata huduma kwa muda mfupi na inatolewa kwa nchi chache barani Afrika.



Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi Mkoa wa Dodoma, Janne Mgidange, akizungumza na washiriki kwenye mafunzo ya ushawishi na utetezi kwa ajili ya viongozi wa asasi za kiraia, jijini Dodoma jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

# RC aipa RUWASA dira kufikia malengo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameitaka Wakala wa Waji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Dodoma kuhakikisha katika bajeti yake kwa mwaka 2021/22 inakutana na kila halmashauri ili kujua mahitaji yake na kupunguza uhaba wa maji kwa wananchi.

Dk. Mahenge aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha wadau wa sekta ya maji na usafi wa mazingira vijijini mkoani hapa iliyoandaliwa na RUWASA kwa lengo la kushirikiana na wadau katika kumaliza tatizo la maji.

Alisema kuna haja ya RUWASA kurudi katika halmashauri ili kupata mahitaji halisi ya miradi ya maji kabla ya kupanga bajeti ya kutekeleza miradi mbalimbali katika Mkoa wa Dodoma.

"Mrudi kwenye halmashauri kule chini wao ndio wanajua mahitaji halisi katika vijiji ili mnapopanga bajeti yenu ilenge katika maeneo yenye uhitaji. Pia katika kila wilaya hakikisheni kuna bwawa ambalo litahudumia vijiji viwili vitatu," alisema.

Pia aliitaka RUWASA kuhakikisha inapita kijiji hadi kijiji ili kuona hali ya upatikanaji wa maji na mahitaji yake halisi ili kuingizwa katika mpango kazi wao katika bajeti ijayo ya wakala.

Alisisitiza kuwa wabunifu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea na katika malengo yao wahakikishe kila kijiji kinapata maji na kuongeza mtandao wa maji kwa wananchi ili huduma hiyo ipatikane kwa urahisi kwa wananchi.

"Lazima tuwe wabunifu kitengo cha ubunifu kiboreshwe kwani Dodoma tuna maji sana chini ya ardhi na kipindi hiki cha mvua tunapoteza maji mengi sana, tukiwa wabunifu haya maji yanayopotea yangesaidia sana," alisema.

Naye Meneja wa RUWASA Mkoa wa Dodoma, Dk. Godfrey Mbabaye, alisema lengo la kikao hicho ni kukutana na wadau na watumiaji wa maji katika halmashauri zote za mkoa ili kushirikishana katika mipango waliyoiweka kuona kama inatija katika maeneo wanayotoka wadau hao.

Alisema RUWASA ina miradi 167 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi 100 imekamilika sawa na asilimia 60.

Dk. Mbabaye alisema hadi Desemba, mwaka jana, utoaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa vijijini ni asilimia 61.9 katika wilaya zote za mkoa na kubainisha kuwa hadi Juni, mwaka huu, hali ya upatikanaji wa maji itaongezeka hadi asilimia 67.2.

Alisema RUWASA Mkoa wa Dodoma kwa mwaka 2020/21 imetengewa zaidi ya Sh. bilioni 9.3 na mpaka Desemba, mwaka jana, ilipokea zaidi ya Sh. bilioni 4.1 sawa na asilimia 44.6.

# Waliokumbwa mafuriko wadai wamesahauliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Mtube Kata ya Nkuhungu, jijini hapa waliokumbwa na mfuriko na kuhama makazi yao wameilalamikia Serikali ya mkoa kwa kuwatelekeza bila kuwapatia msaada wowote.

Wakazi hao walitoa malalamiko hayo jana walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari juu ya hatima yao toka wakumbwe na mafuriko hayo kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa.

Mmoja wa wakazi hao, Rose Kiondo, alisema hivi sasa wana wakati mgumu kutokana na maji kujaa katika makazi yao hali inayowalazimu kuhama nyumba zao.

Alisema kuwa tatizo hilo limetokea muda mrefu lakini hakuna suluhisho ambalo wamepatiwa kutoka katika serikali yao ya mkoa. "Ni muda sasa umepita viongozi wamekuwa wakija na kudai kuwa watakuja kuangalia namna ya kuyaondoa haya maji katika makazi lakini kila wakiondoka hakuna anayerudi na sisi na familia zetu tunaendelea kupata adha kama hii," alisema Kiondo.

Pia alisema kutokana na mafuriko hayo hata biashara zake zimekosa wateja hali ambayo inasababisha kuyumba kiuchumi.

"Wateja wote wamekimbia eneo hilo lakini pia hata wale waliopangisha vyumba wamehama makazi hivyo hivi sasa hali ni ngumu sana kwetu tunaomba serikali itusaidie kutafuta namna ya kuyaondoa haya maji" alisema.

Naye Loy Mhami alisema kutokana na maeneo hayo kujaa maji kila siku majira ya usiku wanalazimika kuwa macho ili kutoa msaada kwa majirani ambao maji yanaingia ndani.

"Mvua hivi sasa zinaendelea kunyesha hivyo usiku hatulali tunasaidia majirani ambao maji yanaingia ndani kwao na kuanza kuhamisha vyombo pamoja na watoto wadogo" alisema Mhami.

Pia alisema hivi sasa hata kazi za kujipatia kipato wanashindwa kuzifanya kutokana na kuwa na kazi moja ya kulinda watoto wasizame kwenye maji.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alitembelea waathirika hao na kuagiza kamati iundwe ili kufanya tathimini

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema suluhisho katika eneo hilo ni kuwaondoa baadhi ya watu na kuwapatia viwanja katika eneo lingine na kwamba tayari wametenga viwanja kwa ajili ya wakazi hao.





## Sababu viongozi kuwa na mgongano kimaslahi zatajwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma Mkoa wa Mbeya, imeeleza mambo mbalimbali yanayosababisha viongozi wa umma kuonekana kuwa na mgongano wa maslahi kwenye utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kanuni za kudhibiti mgongano huo.

Ofisa kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma mkoa wa Mbeya, Lumuli Kibona, aliyataja mambo hayo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu madhara ya viongozi wa umma kuwa na maslahi binafsi wanapofanya maamuzi.

Alisema baadhi ya mambo ambayo yanaashiria kuwa kiongozi ana maslahi binafsi na jambo analolifanyia maamuzi kuwa ni pamoja na kushiriki kwenye mchakato wowote wa kutoa maamuzi yanayohusu mamlaka, majukumu ama kazi ya ofisi bila kuzingatia sheria na kanuni.

Vilevile, alisema kiongozi anaweza kujulikana kwamba ana mgongano wa maslahi endapo atatumia wadhifa wake kujipatia manufaa ama kumsaidia mtu mwingine kupata manufaa kinyume na sheria pamoja na taratibu.

Alisema endapo kiongozi wa umma atatumia taarifa alizozipata katika utekelezaji wa kazi zake ambazo hazijawekwa wazi kwa umma kwa ajili ya kujipatia manufaa ama kumsaidia mtu mwingine ataonekana kuwa na mgongano wa maslahi.

"Pia endapo kiongozi atashiriki katika mchakato wa kutoa maamuzi kwa jambo lolote ambalo linamhusu yeye mwenyewe, kampuni yake au mtu yeyote mwenye uhusiano naye kama mwenza, mtoto au ndugu, kiongozi huyo ataonekana kuwa na maslahi binafsi," alisema Lumuli.

Hata hivyo, alisema kiongozi anaweza akaonekana kuwa na mgongano wa maslahi endapo atatumia wadhifa wake kumsaidia mtu ama kampuni binafsi kujihusisha na serikali katika mazingira yatakayosababisha upendeleo.

Lumuli alisema viongozi wa umma wana wajibu wa kutamka maslahi binafsi kwa Kamishna wa maadili iwapo maslahi hayo ni kinyume na utekelezaji wa majukumu yake. Alisema endapo Kamishana wa Tume ya Maadili atabaini kuwa maslahi yaliyotamkwa na kiongozi wa umma yanaweza yakaathiri utekelezaji wa majukumu ya kiongozi huyo, ataishauri mamlaka ya kinidhamu ya kiongozi huyo ili imuelekeze namna ya kuondoa mgongano wa maslahi.

Alisema mgogoro wa maslahi usipotatuliwa mapema unaweza ukaathiri utendaji kazi wa kiongozi yeyote hasa kwenye hatua ya utoaji wa maamuzi.



Baadhi ya vijana wakiwa wamening'inia kwenye gari ndogo la kubeba mizigo aina ya Kirikuu, jijini Mbeya juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Msongamano wafungwa wanawake gerezani wamshtua Naibu Waziri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, ameonyesha kukerwa na msongamano wa wafungwa wanawake katika Gereza la Ruanda, jijini hapa na kuahidi kuanza kushughulikia tatizo hilo haraka.

Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, alibaini hali hiyo juzi alipofanya ziara katika gereza hilo na kuambiwa na Mkuu wa gereza hilo la wanawake, Mrakibu Mwandamizi wa Magereza, Rehema Mwailunga, kuwa wafungwa hao wanalazimika kulala wengi kwenye chumba kimoja kutokana na uhaba wa mabweni.

Alisema awali mabweni wanayolala wafungwa wanawake hao yalikuwa yanatumika kama selo ya watu waliokuwa wamehukumiwa adhabu ya kunyongwa, lakini kwa sasa yanatumika kwa ajili ya wanawake hao wahalifu.

"Chumba kimoja kilitakiwa kutumiwa na wafungwa watatu, lakini kwa sasa wanalala wafungwa wanawake wanane kwenye chumba kimoja kutokana na ufinyu wa mabweni unaosababishwa na matatizo tofauti tofauti," alisema Mwailunga.

Alisema kwa sasa gereza hilo lina wanawake 38 ambao baadhi yao ni wafungwa na wengine ni mahabusu ambao kesi zao zinaendelea kusikilizwa mahakamani na kuomba mahakama kuongeza kasi ya kusikiliza kesi ili kupunguza mrundikano huo.

Naibu Waziri Mahundi aliahidi kushirikiana na wadau mbalimbali kutafuta vifaa kwa ajili ya ujenzi wa bweni katika gereza hilo ili kuondoa msongamano wa wafungwa kwenye mabweni.

Aliuomba uongozi wa magereza Mkoa wa Mbeya kuweka utaratibu mzuri ambao utasaidia kujengwa mabweni ya gharama nafuu ili wafungwa hao waishi kama binadamu. "Tutawaomba wadau watusaidie, atakayesaidia mabati au saruji sawa, lakini ifahamike kuwa kuja huku haimaanishi kwamba ubinadamu wako unakuwa umeisha, hapana hawa hawatakiwi kuishi kwenye mateso hivi," alisema Mahundi.

Alisema gerezani ni sehemu ya kurekebishana tabia kwa wale wanaokiuka taratibu mitaani na baadhi yao huwa wanabadilika wakimaliza adhabu zao.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, alisema kuna uwezekano wafungwa hao wakaachiwa huru kwa kumaliza vifungo vyao ama kwa msamaha na kurejea mitaani. Alisema wakiwa gerezani wanajifunza stadi mbalimbali ambazo zinaweza zikaja kuwasaidia kuendesha maisha yao mitaani watakapokuwa wameachiwa huru. "Kuwa huku haimaanishi kuwa ndio mwisho, ndio maana hata maaskari wetu wanapokuwa na watu wetu huku wanawafundisha stadi mbalimbali, kwa hiyo niwaombe kwamba wasikate tamaa wala kujihisi wao ni tofauti na watu wengine," alisema Dk. Tulia.

Kwa upande wake, Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Lightness Ndelwa, alisema atawasilisha hoja ya mlundikano wa wafungwa katika gereza hilo ili jiji hilo pia litoe msaada wa kuondoa tatizo hilo.

# Vijana kaya maskini wapewa mafunzo usindikaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA 19 wanaotoka kwenye kaya maskini mkoani Mbeya, wamepatiwa mafunzo ya usindikaji wa vyakula, mboga, utengenezaji wa batiki kisha wakapatiwa zana za kufanyia kazi hizo kwa lengo la kuwakwamua kiuchumi.

Mafunzo hayo ya mwezi mmoja yaliwahusisha vijana kutoka katika halmashauri mbili za Mkoa wa Mbeya ambazo ni Kyela na Mbeya na yametolewa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO).

Yametolewa chini ya ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), ikishirikiana na Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), kwa lengo la kuwasaidia vijana hao kuanzisha miradi yao.

Meneja wa SIDO Mkoa wa Mbeya, Henriko Mdede, alisema walikabidhiwa vijana 19 kwa ajili ya kuwapatia mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali baada ya uchambuzi.

"TEA kwa kushirikiana na TASAF walifanya kazi ya uchambuzi wa vijana hawa kabla ya kuwagawa kwenye vyuo na sisi SIDO Mbeya tulipatiwa vijana 19 ambao wote wamehitimu vizuri mafunzo haya na wanakabidhiwa vyeti na vifaa," alisema Mdede.

Alisema pamoja na mafunzo ya usindikaji wa vyakula, mboga na utengenezaji wa batiki, pia walifundishwa ujasiriamali ili kuwasaidia kuwa na mbinu za kutafuta masoko ya bidhaa watakazokuwa wanazalisha.

Akifunga mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwaasa vijana hao kwenda kuanzisha miradi ambayo wataiendesha kisayansi ili kukuza uchumi wa familia zao pamoja na taifa kwa ujumla.

Alisema vijana hao bado wana umri mdogo na wakifanya kazi kwa bidii na kuzalisha bidhaa bora watakuwa na uwezo mkubwa wa kukua kiuchumi na watakuwa miongoni mwa waajiri wa vijana wengine.

Chalamila aliwataka vijana hao kuepuka makundi yatakayowapotosha na kusababisha shughuli zao kutoendelea au kufa kabisa jambo ambalo litakuwa kinyume na malengo ya wafadhili wa mafunzo hayo.

"Ukizalisha bidhaa bora ni lazima utafanya biashara vizuri, lakini unatakiwa kuwa na lugha nzuri ya kuvutia wateja, umri wenu bado ni mdogo kwa hiyo msije mkaanza kujiunga na wanaowashauri kujishughulisha na ushirikina, ukifanya biashara kishirikina utakuwa mtumwa maisha yako yote," alisema Chalamila.

Alisema serikali itakuwa tayari kuwaunga mkono vijana ambao wataonyesha nia ya kufanya maendeleo ikiwamo kuwasaidia kupata mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo hutolewa na halmashauri.

# Mwinyi amwahidi Dk. Bashiru ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameahidi kumpa ushirikiano Balozi Dk. Bashiru Ally, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Muungano ili aendelee kutekeleza vyema majukumu yake.

Aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na Dk. Bashiru alipofika Ikulu jijini Zanzibar kwa lengo la kujitambulisha kwa Rais kutokana na kuteuliwa kushika wadhifa huo.

Rais Mwinyi alisema yeye na viongozi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) wataendelea kumpa ushirikiano mkubwa kwa azma ya kufanikisha majukumu yake ipasavyo.

Pia alimpongeza Balozi Dk. Bashiru kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na kueleza matumaini yake makubwa kwa kiongozi huyo kutokana na kuutambua uchapakazi wake mahiri alio nao.

Naye Dk. Bashiru alisema ana mategemeo makubwa kwamba ataendelea kupata ushirikiano kutoka SMZ na viongozi wake wote.

Balozi Kakurwa alimwahidi Dk. Mwinyi kwamba atahakikisha ushirikiano unaimarika zaidi kati yake na Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, ili shughuli zao ziende sambamba.

Mapema, Dk. Bashiru alikutana na kufanya mazungumzo na Mhandisi Zena ofisini kwake, Ikulu Zanzibar.

Katika mazungumzo hayo viongozi hao kwa pamoja waliahidi kuimarisha ushirikiano uliopo sambamba na kuendelea kuratibu shughuli zao.

Dk. Bashiru aliteuliwa na Rais John Magufuli Februari 26, mwaka huu, kushika wadhifa huo pamoja na kumteua kuwa Balozi na hatimaye kuapishwa Februari 27, jijini Dar es Salaam.

Balozi Bashiru ambaye Mei, 2018 aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM akichukua nafasi ya Abdulrahman Kinana, kabla ya nyadhifa hizo alikuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhammed Mussa (katikati), akikata keki kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, iliyoandaliwa na uongozi wa Hoteli ya Park Hyatt Zanzibar jana. Watatu kulia ni Meneja ya hoteli hiyo, Nicolas Cedro. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZBS yawahakikishia ubora watumiaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Viwango Zanzibar (ZBS) imewahakikishia wananchi kuwa bidhaa zote zitakazozalishwa nchini kuwa na viwango bora ili kumlinda mlaji zikiwamo za kilimo cha mboga na matunda.

Akifungua mafunzo kwa watendaji wa ZBS yanayohusu usalama wa chakula, Maruhubi mjini Zanzibar, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Rahima Ali Bakar, alisema taasisi imekuwa ikisimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kutengenezwa kwa kuzingatia ubora ili mtumiaji asipate madhara.

Pia alisema kupatiwa mafunzo itasaidia taasisi na taifa kuwa na vitu vinavyoingia nchi kuwa bora na kulinda afya za watumiaji, hivyo kuwaomba wataalamu hao kuzingatia umuhimu wa mafunzo waliyopatiwa, na kuimarisha ubora wa bidhaa kupitia mkulima.

"Umuhimi mkubwa wa mafunzo haya kuwainua Wazanzibari na kuona bidhaa zao wanazozizalisha zinakuwa katika ubora na wenye kiwango na sasa ZBS tumekuwa na maabara ya kupima bidhaa," alisema.

Rahima alisema kupatiwa vifaa kwa kupimia ubora wa bidhaa kutasaidia pia kuona bidhaa zinazozalishwa kuwa na kiwango kizuri na kumlinda afya ya mtumiaji na mlaji kupitia mradi huo.

Naye Meneja wa mradi unaojulikana kwa jina la Kujenga Daraja Kati la Sekta Binafsi na Sekta ya Umma kutoka Taasisi ya Trias, Vicky Macha, alisema malengo wa mradi huo ni kuwafikia zaidi ya wananchi 10,000 wakiwamo wanawake.

Pia alisema lengo kuu la mradi huo ni kuengeza ajira, kipato kwa wakulima na wadau waliokuwapo katika kilimo.

Alisema mradi huo unatarajiwa kufikia shehia 66 ndani ya mikoa mitano na wilaya 10 kwa Unguja na Pemba na wamekuwa wakiangalia makundi manne ya vyakula vikiwamo pilipili hoho, matikiti maji, nyanya na ndizi.

Mratibu wa Usalama wa Chakula na Viwango kutoka Chama cha Wakulima wa Mboga na Matunda (TAHA), Naimana Daniel, alisema katika mafunzo hayo, watahakikisha lengo lililokusudiwa linafikiwa ili kuona viwango vya bidhaa zinaendelea kuwa na ubora zaidi hasa katika kulinda afya za walaji.

## Wanawake watakiwa kujiamini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohammed Mussa, aliwataka wanawake kuungana katika kuitetea jinsia yao kwa kuachana na mila za kuamini kuwa kufanya kazi katika sekta ya utalii kwa wanawake ni kinyume na mila na desturi zao.

Akizungumza katika hafla ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyoandaliwa na Hoteli ya Park Hyatt iliyofanyika katika hoteli hiyo Shangani mjini Zanzibar, alisema jamii inapaswa kufahamu kuwa jinsia zote zina haki ya kufanya kazi zilizo halali kwa lengo la kutengeneza maslahi yao.

Lela alisema bado jamii imekuwa ikitawaliwa na dhana mbaya kuhusiana na sekta ya utalii ikiamini kuwa mwanamke akiingia ni kwenda kinyume cha mila na desturi.

Alisema wanawake wanajitambua na imeonekana kufanya vizuri katika ajira mbalimbali bila kuharibu mila, silka, desturi na utamaduni.

"Niwaombe wanawake wezangu njooni katika sekta ya utalii ili mpate maendeleo," alisema.

Aidha, alisema utafiti uliofanyika duniani unaonyesha kuwa dhamana nyingi walizopewa wanawake kuzifanyia kazi wamekuwa wakifanya vizuri zaidi kuliko wanaume, hivyo hakuna haja ya kuendelea kuvunjana moyo.

Naye Meneja Mkuu wa Park Hyatt, Nicolas Cedro, alisema hoteli hiyo inathamini sana utendaji wa kazi kwa jinsia zote na wana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi. Alisema wanawake ni watendaji wazuri na wanapopewa majukumu ya kazi hufanya kazi kwa uadilifu na uaminifu.


Meneja Rasilimali Watu wa Hoteli hiyo, Catherine Msuya, alisema watahakikisha wanaongeza nafasi za uongozi kwa wanawake na kwamba kwa sasa wako zaidi ya asilimia 20.

"Ushiriki wa wanawake katika uongozi ni jambo muhimu hivyo tutahakikisha tunafikia asilimia ya 50 kwa 50 katika kuwapa nafasi wanawake katika hoteli yetu," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ARIEL NDANSHAU MICHAE**L anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index number **S4104/0087** kilichotolewa na **LORD BADEN POWEL HIGH SCHOOL** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Control No. 9910820255190.**

**IN THE HIGH COURT THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DOSTRICT REGISTRY OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**

**MISC. LAND CASE APPEAL NO 17/2019.**
**[Arising from land Revision No 08/2015 of the DLHT at Bukoba and Originating from Kahororo Ward Tribunal Civil Case No. 11/2015)**

**JAMES BONIPHACE .........APPELLANT VERSUS**
**WARDA ANAORD KISIRAGA....................................RESPONDENT**
**DORIS ELIZUWANI HELMAN .........RESPONDENT**
**TO**
**WARDA ANORD KISIRAGA**
**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant lodged the Appeal against you and registered as Misc.Land Case Appeal No. 17/2019.
Take Notice that the above said appeal has been fixed for mention on 11th March, 2021 at 8:30 Am before Hon. NTEMI N. KILEKAMAJENGA , J. you are ordered to appear in person or through your Advocate
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence
Give under my hand and seL of this Court this 23thday of February, 2021

**J.M Minde**
**DEPUTY REGISTRAR**
**BUKOBA**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **Richard D. Mkama** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki namba **MC 500 BSL** aina ya Boxer. Taarifa imetolewa katika kituo cha Polisi Bukoba kwa jarada namba **KAG/BUK/RB/348214/202**0.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu naye.

**NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI**
**REGENCY GROUP LIMITED**
**KAMPUNI NAMBA 111281**
**NOTISI YA MWEZI DESEMBA 2020**

MWENYEKITI ALIITISHA KIKAO KAMA ILIVYOSTAHILI NA WAHUSIKA WOTE WALIKUWEPO NA MKUTANO HUO ULIFANYIKA TAREHE 20th DESEMBA, MWAKA 2020, SAA 5:00 ASUBUHI NA MAKUBALIANO YAFUATAYO YALIFIKIWA:
WAHUSIKA WALIKUBALIANA KATIKA KIKAO HICHO KWA HIYARI YAO KUWA KAMPUNI HIYO IWE IMEFUNGWA TOKA TAREHE YA KIKAO 20/12/2020 NA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YEYOTE AMBAZO ZITAKUWA ZINAENDESHWA KWA JINA AU KATIKA KAMPUNI.
KAMA MWANAHISA YEYOTE ATAKUWA NA LOLOTE JUU YA MAAMUZI HAYA ANATAKIWA AANDIKE BARUA YA KUPINGA MAAMUZI HAYA KWA MSAJILI WA MAKAMPUNI BRELA NDANI YA SIKU 21 KUTOKA TAREHE YA NOTISI HII.
HIVYO BASI MWENYEKITI ALITOA TAMKO KWAMBA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOENDESHWA KATIKA KAMPUNI.
MKUTANO ULIFUNGWA MNAMO SAA 9:30 MCHANA.

**MAHALI: ARUSHA**
**Tarehe: 20/12/2020**

**ABDULKARIM AHMAD DAKIK**
**Mwenyekiti wa Bodi**

**WEMA MUNUO**
**Sekretari wa Bodi**

**NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI**
**ASEEL GROUP LIMITED**
**KAMPUNI NAMBA 73852**
**NOTISI YA MWEZI DESEMBA 2020**


MWENYEKITI ALIITISHA KIKAO KAMA ILIVYOSTAHILI NA WAHUSIKA WOTE WALIKUWEPO NA MKUTANO HUO ULIFANYIKA TAREHE 20 DESEMBA, MWAKA 2020, SAA 5:00 ASUBUHI NA MAKUBALIANO YAFUATAYO YALIFIKIWA:
WAHUSIKA WALIKUBALIANA KATIKA KIKAO HICHO KWA HIYARI YAO KUWA KAMPUNI HIYO IWE IMEFUNGWA TOKA TAREHE YA KIKAO 20/12/2020 NA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YEYOTE AMBAZO ZITAKUWA ZINAENDESHWA KWA JINA AU KATIKA KAMPUNI.
KAMA MWANAHISA YEYOTE ATAKUWA NA LOLOTE JUU YA MAAMUZI HAYA ANATAKIWA AANDIKE BARUA YA KUPINGA MAAMUZI HAYA KWA MSAJILI WA MAKAMPUNI BRELA NDANI YA SIKU 21 KUTOKA TAREHE YA NOTISI HII.
HIVYO BASI MWENYEKITI ALITOA TAMKO KWAMBA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOENDESHWA KATIKA KAMPUNI.
MKUTANO ULIFUNGWA MNAMO SAA 8:30 MCHANA.

**MAHALI: ARUSHA**
**Tarehe: 20/12/2020**

**MAIN MOHAMAD NASSER**
**Mwenyekiti wa Bodi**

**AHMAD MAIN NASSER**
**Sekretari wa Bodi**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ASHIRAF ISMAILI KAMBENGA** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 187369** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 06/09/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/R-B/135587/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA.129 OF 2020**
**SHABANI MOHAMED MASAWILA......MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**AMINA ABDALLAH SHOMARI.......MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA AMINA ABDALLAH SHOMARI**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 15/04/2021 wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukuosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautohudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetokea kwa mkono wangu leo tarehe 22 mwezi february 2021.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NO 141/2020**
**MADAI ZAMOYONI RICHARD NKOOKO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA FIKIRI ZUBERI**

**KWA FIKIRI ZUBERI**

**Ombi la Mdai ZAMOYONI RICHARD NKOOKO**
**Madai ya pesa sh.3,300,000/=**
**Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauril tajwa hapo juu bila kukosa.**
**Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 15Mwezi 3 Mwaka 2021 saa 8:30 Asubuhi.**

Angalia Kama*hukuhudhuria/hamtohudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha Kama Umepokea/ Mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Màhakama hii leo tarehe 19 Mwezi 02 Mwaka 2021

**PUBLICATION SUMMONS**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATES COURT OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**

**LAND APPEALS NO 24 OF 2019.**

**(Arising from Bukoba District Land and Housing Tribunal Application No. 208/2014)**

**AHMAD SADALLAH KAYAMBA ......APPELLANT**
**VERSUS**
**ALBERT KAKYAIJA ............RESPONDENT**
**NOTICE OF MENTION**

**TO: ALBAERT KAKYAIJA**

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for Mention on the **17TH** day of **MARCH, 2020 at 8:30 o'**clock in the forenoon, before **Hon. J.E.MASSESA – PRM.** Your presence is therefore required on the date and time indicated.
Given under my hand and the seal of the court this **5TH day of MARCH, 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Wataja kikwazo vyumba huduma

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya waganga wafawidhi katika zahanati za Halmashauri ya Mji wa Kibaha wametaja kikwazo cha ufinyu wa vyumba vya kutolea huduma na kusababisha chumba kimoja kuhudumia zaidi ya mtu moja.

Waganga hao waliwasilisha kero zao juzi kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mussa Ndomba, aliyefanya ziara kukagua vituo hivyo vya huduma za afya kujiridhisha hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo hivyo.

Daniel Laizer, Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mwendapole na Salimu Mohamed wa Misugusugu, walisema wakati mwingine wanalazimika kusitisha huduma kupisha mjamzito ajifungue kutokana na kukosekana na chumba maalumu cha kujifungulia.

Waliomba maboresho yafanyike ikiwa ni pamoja na ujenzi wa chumba maalumu cha kujifungulia kwa wajawazito ili wawe na vyumba vya kutosha kwenye zahanati hizo na kuondoa adha wanayokumbana nayo kwa sasa.

Kero nyingine iliyotajwa ni uhaba wa watoa huduma ambayo imechangiwa na ongezeko la wateja katika zahanati hizo na usafiri inapotokea dharura ya kupeleka wagonjwa hospitali ya rufani.

Ndomba alisema amepokea kero hizo na kuahidi kuzishughulikia kwa kuzifikisha ngazi husika ili kuzitafutia ufumbuzi.

Aliwaagiza wahudumu wa afya kwenye vituo hivyo kutoa huduma nzuri na uadilifu kwa wananchi.

Ndomba aliridhishwa na hali ya dawa katika zahanati na vituo alivyotembelea ikiwamo zahanati ya Kongowe, Mwendapole, Misuguaugu na Visiga.

Hali ya dawa kwa sasa katika vituo hivyo alivyotembelea inaelezwa kuwa ni asilimia 80 hadi 90 na dawa hizo zinanunuliwa kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwamo papo kwa papo, Mfuko wa Pamoja (HSBF), Bima ya Taifa (NHIF), Bima ya Afya ya (CHF) na fedha kutoka Serikali Kuu kupitia akaunti ya zahanati iliyopo MDS.

# Asimulia mwanafunzi mwenzao alivyoozeshwa

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

MWANAFUNZI Rozalia Petro anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Ulowa, katika Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, ameelezea namna mwenzake alivyokatishwa masomo na kuolewa ndoa ya utotoni.

Akizungumza na Nipashe kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mapema wiki hii, yaliyofanyika mkoani Shinyanga, Petro alisema mwaka jana walishuhudia mwenzao akiacha masomo na kuolewa.

Wakati wakiwa kidato cha pili mwaka jana, alisema mwenzao (jina limehifadhiwa), walipokuwa wakiendelea na masomo, wazazi wake walikuwa wakipanga mahari yake, ili aolewe na mwanamume ambaye hata hamjui.

Alisema alishuhudia mwenzao ambaye alikuwa mwanafunzi akikamatwa na marafiki wa familia iliyomuoa na kutokomea naye kusikojulikana na kuanzia siku hiyo akawa ameolewa.

"Tunaiomba sana serikali, sisi wanafunzi wa kike, ikomeshe vitendo hivi vya mila na desturi kandamizi za kutomthamini mtoto wa kike, ambavyo vinasababisha kutotimiza ndoto zetu na kuishia kuozeshwa na wazazi wetu kwa tamaa ya kupata mali na mifugo," alisema Petro.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, akizungumza kwenye siku hiyo ya wanawake, alikemea tabia ya baadhi ya wazazi kukatisha masomo watoto wao na kuwaozesha watoto wao ndoa za utotoni kuwa serikali itaendelea kuwa shughulikia.




Ofisa wa Benki ya KCB Tanzania tawi la Zanzibar, Harrison Mashauri (kulia), akiwaonyesha waandishi wa habari baadhi ya vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 5. Kwa ajili ya kuboresha biashara ya Aisha Mohammed (katikati) ambaye ni mmoja wa wanufaika wa programu ya ujasiriamali ya tujiajiri inayoendeshwa na benki hiyo. Kushoto ni Ofisa wa benki hiyo, Evance Charles.

# Vituo vyaja uhakiki bidhaa kwenda nje

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imepanga kuanzisha vituo vya kuhakiki ubora wa bidhaa kabla ya kupelekwa nje ya nchi.

Akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa wadau wa biashara kutoka sekta mbalimbali, Naibu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) aliyemwakilisha Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Emmanuel Munisi, alisema kukosekana kwa vituo hivyo nchini kumekuwa kukichangia kurudisha nyuma uendeshaji wa biashara hizo.

Alisema vituo vya kuongeza na kuhakikisha ubora vitasaidia kufanya uhakiki huo na kuwapunguzia usumbufu wafanyabiashara kusafiri kwenda nje kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo.

"Kitendo cha wafanyabiashara kwenda kuhakiki bidhaa zao nje ya nchi kwa ajili ya kujua kama zina ubora wa kimataifa kulikuwa kunawachelewesha na kuwachukulia muda mwingi wao kufanya biashara zao, kwa hiyo kwa kuanzisha vituo hivyo hapa, vitawapunguzia usumbufu na pia utachangia kasi ya uendeshaji wake," alisema Dk.Munisi.

"Vituo hivyo tunavianzisha na kesho (leo) tutafungua chama kimojawapo cha kuhakiki ubora huo wa bidhaa za kwenda nje ya nchi na kabla ya kuingia nchini."

Dk. Munisi alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali za kuondoa vikwazo katika biashara ikiwamo kuondoa tozo.

"Wafanyabiashara wote wanatoka katika sekta binafsi ambayo ndiyo injini ya maendeleo na uchumi wa nchi na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi mbalimbali tayari imeondoa tozo 170 ambazo zilikuwa zinachangia wafanyabiashara kushindwa kuingiza na kupeleka bidhaa nje ya nchi," alisema Dk. Munisi.

Mratibu wa mradi wa kuwasaidia wakulima kuongeza thamani ya mazao na namna ya kufikia masoko (MURKUP), Safari Fungo, alisema katika utafiti huo ambao umefanywa na wafanyabiashara hao, wamebaini asilimia 50 ya changamoto zilizopo kwenye biashara zipo kwa wafanyabiashara hao kushindwa kukidhi mahitaji ya soko ya ubora na viwango kwenye masoko ya nje.

Kikwazo kingine ni uwapo wa sheria, kanuni na taratibu zisizoendana na uendeshaji wa biashara hiyo hususani katika eneo la uendeshaji za kutoa nje kuingiza nchini na zile za kupeleka nje ya nchi.

## HABARI MICHEZO



# LOW KUACHIA NGAZI UJERUMANI

**MUNICH,** Ujerumani

IMERIPOTIWA kuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low, ataachana na timu hiyo mapema mwaka huu.

Low ameamua kusitisha mkataba wake na timu hiyo na ataachia nafasi hiyo baada ya mashindano ya Euro 2021.

Low amekuwa muhimili mkubwa kwenye timu ya Taifa ya Ujerumani kwa muda wote aliokuwa kocha mkuu wa timu hiyo na kufanikiwa kutwaa Kombe la Dunia mwaka 2014.

Kabla ya taarifa hiyo, kulizuka maneno ya chini yaliyomhusisha kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp kwamba, huenda akavutiwa zaidi na nafasi ya kukinoa kikosi cha Ujerumani endapo Low ataondoka.

Low amekuwa akishutumiwa kwa siku za hivi karibuni kutokana na mwenendo mbovu wa timu hiyo.

Kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 nchini Urusi, Ujerumani ilitolewa hatua ya makundi na hivyo kujikuta kwenye wakati mgumu.

# Cavani kuondoka Manchester United

**MANCHESTER,** England

BADO kuna hali ya sintofahamu kuhusu hatima ya mshambuliaji wa Manchester United, Edinson Cavani.

Mkataba wa mchezaji huyu unamalizika mwishoni mwa msimu huu na inasemekana kuna kila dalili za kutoongezewa mkataba mpya.

Kwa sasa Cavani yupo nje ya uwanja kutokana na majeruhi, lakini imeripotiwa kuwa mshambuliaji huyu hafurahii maisha ndani ya Uingereza na hivyo kuna uwezekano akarejea nyumbani kwao Amerika Kusini.

Hii ni baada ya baba mzazi wa mchezaji huyo, Luis Cavani kukiambia kituo cha habari cha Tyc Sport Network kuwa; "kuna asilimia 60 za Edinson kurejea Amerika ya Kusini.

"Tunategemea hilo. Tumekuwa tukimtembelea, amekuwa kwenye maeneo mazuri ambapo watu walimpokea vizuri.

"Amefanya watu wampende, ametengeneza marafiki wengi, lakini leo hafurahii mahali alipo kwa sasa.

"Kwa zaidi ya miaka miwili amekuwa akifikiria kuwa anataka kuwa karibu zaidi na familia na hiyo ni sababu ninayofikiri Edinson ataishia kuchezea timu ya hapa hapa Amerika Kusini."

Kumekuwa na taarifa kuwa huenda Cavani akatimkia kwenye klabu ya Boca Juniors inayocheza Ligi Kuu Argentina na kwa maelezo ya baba yake mzazi, huenda hili likatokea mwishoni mwa msimu huu.






# Tuchel aandika historia Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, jina lake limeingia kwenye vitabu vya historia kwenye Ligi Kuu Engand, baada ya kutofungwa mechi 11.

The Blues hao hawajafungwa katika mechi 11 chini ya Mjerumani huyo, wakati ushindi wa 2-0 kwa Everton Jumatatu ulimfanya kuwa kocha wa kwanza katika historia ya Ligi Kuu kutoruhusu nyavu zake kutikiswa katika kila mechi ya nyumbani.

Matokeo hayo yaliifanya Chelsea kutoruhusu nyavu zao kutingishwa mara tano mfululizo kwenye mechi ya nyumbani za ligi, ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2015.

'Blues' hao wameruhusu mabao mawili tu katika michezo 11 tangu Mjerumani huyo achukue jukumu la kuinoa, na yeye mwenyewe amesema ni juhudi za pamoja.

Mlindamlango wa Blues, Edouard Mendy, alipigiwa shuti moja tu kwenye lango lake, na kwa upande mwingine bao la kujifunga kutoka kwa Ben Godfrey na penalti ya Jorginho ziliifanya Cheslea kupata pointi zote tatu.

HABARI MICHEZO

# Haaland ataleta zama mpya - Lopetegui

**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA Mkuu wa Sevilla, Julen Lopetegui, amesema Erling Haaland "ataleta zama mpya kwenye soka" baada ya nyota huyo wa Borussia Dortmund kutengeneza historia zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Haaland alifunga mara mbili wakati Dortmund ikitoka sare ya mabao 2-2 na Sevilla kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16-bora na kufuzu hatua ya robo fainali kwa ushindi wa uwiano wa mabao 5-4 juzi, Jumanne.

Haaland ambaye amekuwa akihusishwa na timu kama Real Madrid, Chelsea, Manchester City, Manchester United, Barcelona na Juventus – amekuwa mchezaji aliyefikisha mabao 20 kwa haraka zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi 14.

Akiwa na umri wa miaka 20 na siku 231, Haaland pia amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga katika mechi sita mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku pia akiwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya mashindano hayo kufunga angalau mabao mawili kwenye mechi nne mfululizo.

Lopetegui alimsifia Haaland – ambaye pia alifunga mabao mawili kwenye mchezo wa kwanza – akiwaambia waandishi wa habari: "Mwanzo tulicheza vizuri na tulikuwa bora.

"Lakini haikutosha kwa sababu walituadhibu kwenye mchezo wa kwanza, shukrani kwa mchezaji ambaye ataleta zama mpya za soka na ametengeneza tofauti.






# DONNARUMMA AWINDWA NA VIGOGO LIGI ENGLAND

**LONDON,** England

KLABU za Manchester United na Chelsea zimeingia kwenye mbio moja za kuwania saini ya golikipa wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma, kwa mujibu wa Daily Mail.

Donnarumma mkataba wake na Milan unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutotaka kuongeza mkataba mpya

Ingawa Milan bado ipo kwenye majadiliano na golikipa huyo wa kimataifa wa Italia, lakini inaonyesha wazi kuwa yeye mwenyewe anataka kutafuta changamoto mpya.

Na sasa Man United na Chelsea zimeamua kujitosa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania saini ya kipa huyo.

Pia mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus na Paris Saint-Germain ya Ufaransa zimehusishwa naye.

Sky Sports imesema United pia inamwania golikipa namba moja wa Atletico Madrid, Jan Oblak, huku kukiwa na uvumi juu ya majaliwa ya baadaye ya David de Gea.

# *United kumruhusu De Gea kuondoka*

**MANCHESTER,** England


KLABU ya Manchester United imeanza mazungumzo na kipa wake namba moja, David de Gea ili kumsikiliza ofa yake.

Ripoti zinaeleza kwamba United itamsikiliza kipa huyo kile anachokihitaji na itampa ruksa ya kufanya chaguo analotaka yeye, bila kumbana kwa kuwa amefanya nao kazi kwa ukaribu na muda mrefu.

Ikiwa de Gea akaamua kusepa ndani ya kikosi hicho kinachonolewa na kocha Ole Gunnar Solskjaer, itakuwa ni nafasi kwa Dean Henderson kuwa kipa namba moja.

Tayari Solskjaer ameanza kumwamini Henderson kwenye kikosi cha kwanza lengo likiwa ni kumjengea hali ya kujiamini, ili aweze kurithi mikoba ya De Gea ambaye ameanza kikosi cha kwanza kwenye jumla ya mechi 434.

De Gea amekuwa akitajwa kuwaniwa na PSG ya Ufaransa, huku pia Real Madrid nayo ikihusishwa naye.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RIVALDO AITAKA BARCA SASA KUMSAJILI RAMOS

**Bila shaka, utakuwa usajili mzuri sana na itakuwa historia kwa sababu ya historia yake...**

**BARCELONA,** Hispania

RIVALDO anaamini kwamba, nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos, utakuwa usajili mzuri sana kwa wapinzani wao kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona.

**Ramos mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na mlinzi huyo bado hajakubali kusaini mpya na mabingwa hao wa LaLiga.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye ni nahodha wa timu ya Taifa ya Hispania amekuwa akihusishwa na timu kama Manchester United, Manchester City na Juventus.

Rivaldo, ambaye alishinda mataji mawili ya LaLiga wakati akicheza pale Barca, anataka Ramos ahamia kule Camp Nou.

"Mchezaji anatakiwa kuheshimu kazi yake, na kama kuna ofa nzuri, sidhani kama ni jambo baya kuwasikiliza," amesema mchezaji huyo wa zamani wa Brazil akinukuliwa na Betfair. "Bila shaka, Sergio Ramos utakuwa usajili mzuri sana kwa Barcelona. Itakuwa historia kwa sababu ya historia ya Sergio Ramos na Real Madrid."

Ramos amepaita Madrid nyumbani tangu alipojiunga nayo kutoka Sevilla mwaka 2005, akishinda mataji matano ya LaLiga, manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Klabu Bingwa Dunia na mataji manne ya UEFA Super, kati ya mataji 22 aliyobeba pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Pia kumekuwa na uvumi kuhusu majaliwa ya Lionel Messi hapo Barca akihusisha na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Catalunya akiwa huru mwishoni mwa msimu huu.

Messi mshindi mara sita wa Ballon d'Or amekuwa akihusishwa sana na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain na vinara wa Ligi Kuu England, City.

"Kama ningekuwa kocha wa PSG (Mauricio) Pochettino, ningemwambia mmliki wa PSG kwamba, sisi ni bora kabla ya kumleta Messi," alisema Rivaldo.

"Nampenda Messi, lakini (Kylian) Mbappe yupo nyumbani na anafaa zaidi kuendelea kuwa na timu hii.

"Ni ngumu kuzungumza kuhusu mabadiliko kutoka Messi hadi Mbappe, kwa sababu soka ni fedha na kama Messi atakwenda PSG, litakuwa jambo la kujinufaisha kiuchumi.

"Lakini Messi tayari yupo na umri zaidi ya miaka 30 na PSG wana Mbappe mwenye umri wa miaka 22."

## ZISIKUPITE

### DE GEA SOKONI UNITED

MANCHESTER United itasikiliza ofa za kumuuza kipa wake, David De Gea mwenye umri wa miaka 30 mwisho wa msimu huu, huku kocha Ole Gunnar Solskjaer akiwa tayari kumfanya Dean Anderson kuchukua nafasi ya kwanza ya mlinda mlango huyo. ***(90min via Mail)***

### ARSENAL YAMTAKA HAKIMI

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kuwa iko tayari kuchukua fursa ya mzozo unaoendelea katika klabu ya Inter Milan kwa kuwasilisha ofa ya kumnunua beki wa Morocco, Achraf Hakimi. ***(Mirror)***

### AGOMBEWA MANCHESTER

MANCHESTER United na Manchester City zinawania kumsajili beki wa Villarreal na Hispania, Pau Torres, 24. ***(Manchester Evening News)***

### LUNDSTRAM ATAKIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inapanga kumsajili kiungo wa kati wa Sheffield United, John Lundstram, mwenye umri wa miaka 27. ***(Express)***

### MASCARELL AWANIWA WOLVES

KIUNGO wa kati wa Schalke na Hispania, Omar Mascarell mwenye umri wa miaka 28, ameonekana kama mchezaji anayelengwa zaidi na klabu ya Wolves mwisho wa msimu huu. ***(Caught Offside)***

### AGUERO KUBAKIZWA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anatumaini anaweza kumshawishi mshambuliaji wake, Sergio Aguero, 32, kusalia na klabu hiyo. ***(Star)***

### OBLAK AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester inamnyatia golikipa wa Atletico Madrid na Slovenia, Jan Oblak, mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

### MAHREZ ATAKIWA MADRID

REAL Madrid ina nia ya kumsajili winga wa Manchester City na Algeria, Riyad Mahrez, 30. ***(FootMercato)***

### VILLA WAMTAKA HENDRY

MLINZI wa kati wa Celtic na Scotland, Jack Hendry mwenye umri wa miaka 25, ameripotiwa kunyatiwa na klabu ya Aston Villa, kwa dau la pauni milioni 10. ***(Birmingham Mail)***

### ALABA KUTUA BARCELONA

BARCELONA imeafiki makubaliano ya maneno na klabu ya Bayern kumnunua beki wake, David Alaba, 28 raia wa Austria. ***(Mundo Deportivo)***

### MILAN WAMTAKA MANDI

INTER Milan imewasiliana na wakala wa mlinzi wa Ufaransa na Real Betis, Aissa Mandi mwenye umri wa miaka 29, ambaye alikuwa anawaniwa na Liverpool wakati wa usajili wa dirisha dogo la Januari. ***(Calciomercato)***

## Poulsen aanza na washambuliaji

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Kim Poulsen, ameanza kukinoa kikosi chake kujiandaa mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) huku akielekeza nguvu zaidi katika safu ya ushambuliaji.

Taifa Stars imeingia kambini juzi na kuanza mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili ya mchezo dhidi ya Equatorial Guinea kuwania kufuzu Afcon utakaopigwa ugenini Machi 25, kabla ya siku tatu baadaye kuikaribisha Libya hapa nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Poulsen alisema amerídhishwa na idadi ya wachezaji waliohudhuria katika mazoezi hayo na kuanzia na yeye moja kwa moja kuanza na mazoezi ya kufunga kwanza.

## Zimamoto yamulika ushindi 7 za mwisho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya timu ya Kipanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyopigwa Uwanja wa Mau A juzi, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohammed Ali Hilali "Tedy", amesema matarajio yao sasa ni kuendelea kupata ushindi katika mechi saba zilizobaki ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Zimamoto tayari imeshacheza michezo 15 huku ikiwa imebakisha mechi saba kabla ya msimu huu wa 2020/21 kumalizika.

Akizungumza na gazeti hili juzi, kocha huyo alisema katika kipindi hiki cha kuelekea ukingoni mwa msimu wa ligi, kupata ushindi ni jambo la muhimu kwa kuwa timu zote zinacheza kwa kupambana ili zitoke na matokeo mazuri.

# YANGA PRINCESS YAPANIA KUIPOKA SIMBA UBINGWA

**Saada Akida na Shufaa Lymo**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema licha ya kufungwa na Simba Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake, bado hawajaondolewa katika mipango yao ya mbio za ubingwa msimu huu, kauli ambayo iliungwa mkono na straika wa timu hiyo, Aisha Masaka.

Akizungumza na mwandishi wetu Dar es Salaam jana, Edna alisema pamoja na mchezo huo waliopoteza kwa mabao 3-0 wiki iliyopita katika Uwanja wa Uhuru, lbado wanamatumaini makubwa ya kufanyia kazi upungufu wao kuelekea mechi zilizopo mbele yao na kuweza kupata matokeo chanya.

"Ubingwa bado tupo katika mbio hizo na tunaendelea kupambana kutafuta matokeo chanya kwa kila mechi ili kufikia malengo," alisema Edna.

**Alisema ana imani na timu yake kufanya vizuri katika mechi zilizobaki kwa sababu kila mchezaji ana morali ya kutafuta matokeo mazuri.**

Kwa upande wa straika wa timu hiyo, Masaka, alisema utabiri wake wa ubingwa msimu huu, anauelekeza kwa timu yake kwa kuwa wana kikosi bora kinachoweza kupigania kurudi kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Alisema licha ya Simba Queens kuwashusha katika nafasi waliyokuwapo, hawajakata tamaa na badala yake atashirikiana na wachezaji wenzake kurejea kileleni.

"Nina matumaini timu yangu itaendelea kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi yetu kutokana na mazoezi ambayo tunaendelea kuyafanya kila siku tunaomba mashabiki wetu wazidi kutupa ushirikiano," alisema.

Alisema kuna kila uwezekano wa kufanya vizuri katika ligi hiyo kwa kuwa mpaka sasa bado kuna michezo mingi iliyopo mbele yao ambayo anaamini wanaweza kuitumia kupata matokeo mazuri.

Yanga Princess ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake ikiwa na pointi 38, wakati mabingwa watetezi, Simba Queens wakiongoza kileleni kwa alama 39, timu zote zikiwa zimecheza mechi 15 kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

**KAPATIA 12...**




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Joseph Hamisi, kutoka Kigamboni, Dar es Salaam, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 12.8 baada ya kukabidhiwa kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwa muungano wa aina moja kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot kwa sasa imefika Sh. milioni 506. **PICHA: SPORTPESA**

# Twanga Pepeta yatangaza uzinduzi albam mpya

**Na Mwandishi Wetu**

BENDI ya muziki wa dansi ya African Stars maarufu Twanga Pepeta, inatarajia kufanya uzinduzi wa albam yao mpya ya 14 ifikapo Aprili 3, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Break Pointi zamani Kijiji cha Makumbusho jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Uzinduzi huo utaenda sambamba na tamasha la utoaji wa tuzo za wanamuziki litakaloitwa "Tuzo za Wanamuziki Waliotukuka".

Akizungumza jana jijini, Mkurugenzi wa Twanga Pepeta, Asha Baraka, alisema maandalizi ya uzinduzi na tamasha hilo yako katika hatua za mwisho na wamejipanga kufanya onyesho la kihistoria hapa nchini. Asha alisema tayari wamesharekodi nyimbo tano mpya pamoja na video zake na hatua iliyobakia ni kufanya uamuzi wa kibao kitakachobeba jina la albamu hiyo mpya.

"Twanga tumejipanga kurudi katika ubora wake, tumejiandaa kufanya tamasha kubwa na hili la tuzo litafanyika kila mwaka, tunawashukuru wadau na wadhamini wote waliojitokeza na ambao wako njiani kutusaidia ili kufikia malengo," alisema Asha.

Naye Ofisa Mtendaji wa bendi hiyo, Lwiza Mbutu, alisema wanamuziki wote wamejiandaa kutoa burudani ya kiwango cha juu baada ya kufanya maandalizi mazuri kwa muda mrefu.

Lwiza ambaye ni mwimbaji mkongwe wa bendi hiyo, alizitaja nyimbo zitakazokuwapo katika albam hiyo kuwa ni pamoja na 'Twanga Mbele, Rekebisha, Povu, Penzi Sigara Kali na Push to Start'.

"Pia napenda kuwatambulisha wanamuziki wetu ambao wamerejea nyumbani, Victor Mkambi, Khalid Chokoraa, lakini Super Nyamwela sasa naye ni mpiga "drum" namba mbili wa bendi, tena amekuwa katika kiwango cha juu akiongozwa na Ally Ramadhani 'Kirikuu'," alisema Lwiza.

Msafiri Diuof amewataka mashabiki wa bendi hiyo wajiandae kushuhudia burudani nzuri na ambayo hawajawahi kuiona hapa nchini.

"Ninawaambia mashabiki wetu wajiandae kuona kitu fulani 'unique' (chakipekee), tunajiandaa kuwafurahisha, tumedhamiria," Diouf alisema.

Mwakilishi wa maji aina ya Tukuyu Spring, Baraka Mwaijalo, alisema kampuni yake imekubali kudhamini uzinduzi huo kwa sababu wanataka kurejesha heshima na hadhi ya muziki wa dansi hapa nchini kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

# Michezo

Alhamisi Machi 11, 2021

Nipashe




Cavani kuondoka Manchester United UKURASA 20

## DUH! TUMETOKA...



Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, akihuzunika baada ya kukosa bao wakati timu yake ikitupwa nje na FC Porto kwenye mechi ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora iliyopigwa Turin, Italia na kumalizika kwa wenyeji hao kushinda 3-2, lakini wakatolewa kwa faida ya bao la ugenini kutokana na mechi ya awali nchini Ureno, Porto kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Lwanga wa Simba amwamsha Baraza

**Na Shufaa Lyimo**

UWEZO unaoonyeshwa uwanjani katika mashindano mbalimbali na kiungo mkabaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mganda Taddeo Lwanga, umemkuna Kocha Mkuu wa timu ya Biashara United, Francis Baraza, anayetajwa kuwania vikali kwenda kuinoa timu ya Kagera Sugar.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, kocha huyo alisema kiungo huyo akiwa uwanjani anajua kuumiliki mpira ipasavyo ikiwa ni pamoja na matumizi mazuri ya nguvu huku akihakikisha anazuia mashambulizi makali kuwafikia mabeki wao wa kati.

"Taddeo anajituma sana, anapokuwa uwanjani ni moja kati ya viungo ambao wana manufaa makubwa ndani ya timu yake, ni mchezaji ambaye ananivutia sana, hakika klabu ya Simba imesajili mchezaji mzuri," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema unapokuwa na mchezaji kama Lwanga ndani ya timu, inaongeza uimara mkubwa kikosini na kuamsha ari ya kujituma kwa wachezaji wengine wa kikosi cha kwanza.

Alisema mchezaji huyo anatimiza wajibu wake akitambua amekuja Tanzania kwa ajili ya kazi moja ya kucheza mpira, na kwamba hicho ndicho kitu ambacho anakifanya jambo linalowavutia wadau mbali mbali wa soka akiwamo yeye.

# KAZE AWEKA REKODI KALI YANGA, AWAPA DARASA

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Simba haikufurukuta kwake, mechi 23 ushindi 14, asema kama inataka kubeba makombe lazima...

HUKU akieleza kinachotakiwa kufanya kwa klabu ya Yanga ili kuweza kutimiza malengo yake ya kutoa ushindani wa mbio za Ligi Kuu Bara na michuano mingine itakayoshiriki, aliyekuwa Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mrundi Cedric Kaze, ameacha rekodi ya kuvutia kwenye mashindano yote aliyoiongoza timu hiyo, takwimu haziongopi.

**Kaze ambaye alitua Yanga kuchukua nafasi ya Mserbia Zlatko Krmpotic, aliyeanza msimu huu wa 2020/21 akiiongoza timu hiyo kwenye mechi tano za Ligi Kuu Bara na kuiwezesha kushinda michezo minne na kutoka sare moja, Mrundi huyo naye hakufanya vibaya katika mashindano matatu tofauti aliyoiongoza.**

Kwa upande wa Kaze, ameiongoza Yanga jumla ya mechi 23 katika mashindano yote akishinda michezo 14, sare nane na kupoteza mchezo mmoja tu, huku akiipa timu hiyo ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, likiwa taji la kwanza kwa klabu hiyo katika kipindi cha misimu mitatu.

Katika mechi hizo, kwenye Ligi Kuu Bara, Kaze ameiongoza Yanga mechi 18, akishinda 10, sare saba na kupoteza mchezo mmoja pekee, hivyo ameondoka akiiacha timu hiyo ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi kama ambavyo mtangulizi wake Krmpotic alifanya wakati akiachana nayo.

Kwenye Kombe la Mapinduzi, Kaze ameiongoza Yanga mechi nne, akishinda tatu na sare moja wakati kwenye Kombe la FA akiiongoza mchezo mmoja ambao pia wameshinda na kutinga raundi ya 16-bora.

Lakini, Kaze ameondoka akiweka rekodi ya kutofungwa na watani zao, Simba timu hizo zilipokutana kwenye Ligi Kuu Bara mzunguko wa kwanza Novemba 7, mwaka huu, baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya bao 1-1 shukrani kwa bao la Michael Sarpong (kwa penalti) huku la wapinzani wao likifungwa na Joash Onyango kwa kichwa.

Kwa upande wa Kombe la Mapinduzi, Kaze alitwaa taji hilo kwa sifa kubwa ya kuwafunga watani zao, Simba kwa mikwaju ya penalti 4-3 baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare tasa.

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya kusitishiwa mkataba wake na Yanga, Kaze mbali na kushukuru kwa kipindi chake cha furaha cha miezi mitano alichoiongoza klabu hiyo, alibainisha kinachotakiwa ili kuweza kufanya vizuri kwenye mashindano yanayowakabili.

Alisema viongozi walijitahidi kufanya usajili mzuri mwanzoni mwa msimu, lakini bado hawakuwa na wachezaji wenye daraja la juu ambao wanaweza kuziba pengo la mchezaji yeyote anayecheza ndani ya kikosi cha kwanza wanapofanya mabadiliko.

"Pamoja na kwamba viongozi walijitahidi kufanya usajili kwenye dirisha dogo, lakini kwa bahati mbaya huwezi kusajili wachezaji wengi kwenye dirisha dogo, hivyo ili Yanga kuwa bora, lazima isajili wachezaji wa kuweza kushindania namba na nyota wanaoanza kwenye kikosi cha kwanza," alisema.

Yanga ambayo ilivunja benchi nzima la ufundi, imemuita aliyekuwa Kocha Msaidizi, Juma Mwambusi, ambaye alikuwa mapumzikoni kwa zaidi ya wiki tatu akijiuguza, kuja kuiongoza klabu hiyo kwa muda wakati huu Kamati ya Utendaji ikifanyia kazi mchakato wa kumpata kocha mkuu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >